# TASNIA YA KAHAWA TANZANIA

## MKAKATI WA MAENDELEO 2011/2021



TOLEO LA

(2012)

*Ninapenda kuwashukuru sana wajumbe wa Task Force Committee ambao wametumia muda wao mwingi kuhudhuria mikutano ya kila mwezi kuhakikisha mkakati huu unakamilika. Nembo za wajumbe hao zimeorodheshwa chini kialufabeti.*

*Adolph Kumburu*

*Mwenyekiti TFC*

Kwa msaada na ushiriki wa
(Kwa mpangilio wa kialfabeti):

G32 Kilimanjaro New Cooperative Initiative,
Joint Venture Enterprise

**Yaliyomo**

Orodha ya Vifupisho ........ ii

Muhtasari Rasmi ........ 1

Utangulizi ........ 3

1. Muktadha wa jumla wa Sekta ya Kahawa Tanzania ........ 4
   - 1.1 Fursa ya Tasnia ya Kahawa Tanzania katika Masoko ya Dunia ........ 4
   - 1.2 Hali ya Kahawa ya Tanzania ........ 7
   - 1.3 Changamoto kuu zinazoikabili tasnia ya Kahawa nchini Tanzania ........ 15

2. Mkakati wa Maendeleo ya Sekta ya Kahawa: Dira, Madhumuni na Misukumo ya Kimkakati ........ 20
   - 2.1 Dira ya Mkakati ........ 20
   - 2.2 Dhumuni la Mkakati ........ 20
   - 2.3 Misukumo ya kimkakati ........ 20

3. Mpango wa Utekelezaji wa mkakati ........ 24
   - 3.1 Shughuli kuu za utekelezaji ........ 24
   - 3.2 Mfumo wa utekelezaji unaopendekezwa ........ 33
   - 3.3 Upangaji wa vipaumbele na makisio ya awali ya gharama ........ 36
   - 3.4 Mpangilio wa mabadiliko yanayowezekana na matokeo ya mkakati Kijamii na Kiuchumi ........ 41

Viambatanisho ........ 44

**Orodha ya Vifupisho**

| | |
|---|---|
| ASDP | Mpango wa Maendeleo ya Sekta ya Kilimo |
| ASDS | Mkakati wa Maendeleo ya Sekta ya Kilimo |
| CBB | Ugonjwa wa chulebuni wa Kahawa |
| CLR | Kutu ya Majani ya Kahawa |
| CPU | Mashine za kumenyea Kahawa |
| CWD | Ugonjwa wa Mnyauko fuzari wa Kahawa |
| DALDO | Ofisa Kilimo na Maendeleo ya Mifugo wa Wilaya |
| GAP | Kanuni Bora za Kilimo |
| ICO | Shirika la Kimataifa la Kahawa |
| GIS | Mfumo wa Taarifa za Kigrafi |
| MKUKUTA | Mkakati wa Kuimarisha Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania |
| NCC | Mkutano wa Kitaifa wa Kahawa |
| NGO | Asasi isiyo ya Serikali |
| PPP | Ubia wa Umma na Binafsi |
| SACCOS | Chama cha Kuweka na Kukopa |
| TaCRI | Taasisi ya Utafiti wa Kahawa Tanzania |
| TCB | Bodi ya Kahawa Tanzania |
| TSH | Shilingi ya Tanzania |
| TCA | Chama cha Kahawa Tanzania |
| USD | Dola ya Marekani |
| ZSC | Kamati za wadau za Kanda |

**Muhtasari Rasmi**

Kahawa ni mojawapo ya mazao makuu ya biashara yanayosafirishwa nchi za nje, ikichangia kiasi cha 5% ya mapato ya jumla bidhaa zinazosafirishwa nje, na inazalisha mapato ya wastani wa Dola za Marekeni millioni 100 kwa mwaka kwa zaidi ya miaka 30 iliyopita. Tasnia hii hutoa mapato ya moja kwa moja kwa zaidi ya kaya za wakulima 400,000, hivyo, kusaidia utafutaji wa riziki wa watu wanaokadiriwa kuwa milioni 2.4.

Wastani wa uzalishaji wa mwaka kwa zaidi ya miaka 30 iliyopita umesimama kwenye kiwango cha tani 50,000 ambapo uzalishaji unaendelea kupungua na uwezekano wa ubora haukutumika/hauzingatiwi kikamilifu, hivyo kuchangia katika kupata bei ndogo za shambani na kuendeleza umaskini wa vijijini.

Kwa kuzingatia fursa zilizopo kwenye soko la Kimataifa, na uwezekano wa kuzalisha kahawa ya ubora wa hali ya juu, kwenye ngazi ya Kimataifa (ikijumuisha Arabika laini pamoja na Robusta) **Tanzania ingekabiliana na matatizo machache sana katika uuzaji wa kiasi kikubwa cha kahawa kwa bei inayoleta faida sana ili mradi uzalishaji unaongezeka.**

Kwa kutambua fursa hii kubwa, Serikali ya Tanzania pamoja na Wadau wa Tasnia ya Kahawa, chini ya uongozi wa Bodi ya Kahawa imezindua ushirikiano wa Kitaifa ili kukubaliana juu ya Mkakati wa Maendeleo ya Sekta ya Kahawa (2011-2012). Kutokana na mchakato huu shirikishi, wadau wa Kimataifa wa Kahawa wamekubaliana juu ya dira ifuatayo kwa ajili ya mkakati huo.

> *"Bodi ya Kahawa Tanzania inakusudia kujenga tasnia endelevu na yenye faida kwa wadau wote, wanaozalisha kahawa ya Arabika na Robusta yenye ubora wa hali ya juu unaotambulika kimataifa na kutoa mchango mkubwa kiuchumi, kupunguza umaskini na uboreshaji wa riziki ya Watanzania wote."*

Waraka huo unelenga kwenye dhamira ya jinsi ya **kuongeza uzalishaji kutoka wastani uliopo wa tani 50,000 hadi angalau tani 80,000 kufikia mwaka 2016 na kufikia tani 100,000 kufikia mwaka 2021.** Inatarajiwa kwamba ongezeko katika wingi wa uzalishaji litakwenda sambamba na ongezeko katika ubora kutoka 35% iliyopo ya Kahawa ya thamani ya juu hadi angalau 70% ya jumla ya uzalishaji.

Ongezeko la uzalishaji litafikiwa kupitia uboreshaji wa tija ambao utaruhusu faida kwa wazalishaji na hivyo kuhakikisha uendelevu wa kiuchumi. Inakadiriwa kwamba ubadilishaji endelevu wa mibuni ya zamani kwa kupanda aina zilizoboreshwa, pamoja na matumizi ya kanuni bora za kilimo (ikiwa ni pamoja na urengetaji, upogoaji, upaliliaji, uwekaji wa matandazo, utumiaji wa mbolea) utaruhusu kuongezeka kwa +100% wastani wa mavuno kutoka kiwango cha sasa cha kg 225 za Kahawa safi kwa hekta hadi kg 450 za Kahawa safi kwa hekta ifikapo mwaka 2021 (+55% mwaka 2016). Hili peke yake lingesababisha ongezeko kwa kiasi cha tani 50,000 za uzalishaji wa Kitaifa. Kwa sasa, uzalishaji ungeweza kupanuliwa katika maeneo mbalimbali. Jumla ya hekta 10,000 zitapandwa na wakulima wadogowadogo na wawekezaji wakubwa kuanzia sasa hadi mwaka 2021 ikimaanisha angalau hekta 1,000 kwa mwaka. Mkakati huu wa upandaji upya, uzidishaji, na upanuzi unapaswa kwenda sambamba na mpango wa uongezaji miche wa TaCRI ambapo kiasi cha miche milioni 20 lazima kipatikane kila mwaka katika kipindi hiki. Pia, kuna haja ya kuwezesha shughuli za ugani shambani.

Hili linaweza kufanikishwa kwa kupitia Mafunzo kwa wakufunzi na kuwajengea wa uwezo maofisa ugani ili waweze kuhamisha teknolojia kwa wakulima katika vikundi vyao kupitia mafunzo vijijini.

Ili kujenga sekta ya Kahawa yenye ushindani endelevu, ni muhimu sana kuongeza ufanisi wa mnyororo wa thamani kupitia matumizi ya kiwango cha juu kabisa cha mfumo wa soko na uboreshaji wa mazingira ya biashara kwa ujumla. Lengo ni kuzuia uingiliaji kati usio wa lazima na kupunguza gharama za uendeshaji ili wakulima waweze kupata angalau 75% ya bei ya bandarini (FOB) ifikapo mwaka 2021. Faida iliyoboreshwa ya sekta hii itasababisha uimarishaji wa uwezo wa wadau wa tasnia hii kuwekeza katika uboreshaji wa mnyororo wa thamani. Kufikia hapa, mkakati huu unapanga kuanzishwa kwa kanuni zilizoboreshwa, uanzishaji wa mfumo wa taarifa za soko unaofanya kazi na utoaji wa huduma muhimu za ushauri.

Sambamba na hili, kuna fursa za kuongeza ubora kupitia matumizi ya kanuni bora za uvunaji na usindikaji na matunizi ya vifaa na miundombunu bora ya usindikaji ikiwa ni pamoja na Mashine za kati za kumenyea kahawa (CPUs). Hili litaiwezesha Tanzania kufanikisha hadhi yake ya kuwa katika kundi la wazalishaji wa kahawa ya Kolombia laini na kupata bei za thamani ya ubora zaidi katika mnyororo wote wa thamani na hususan, wazalishaji.

Mwisho, mkakati huu unapanga kuongeza uhamasishaji wa Kahawa ya Tanzania katika masoko ya nje ili kuboresha ongezeko la bei ya thamani ya juu pamoja na kutafuta fursa za masoko mapya. Umuhimu unaotolewa na tasnia ya Kimataifa kwa masoko endelevu pia unapaswa kuzingatiwa wakati wadau wakuu wanaoongoza duniani wanaendelea kuhimiza kuongeza wigo wa Kahawa endelevu katika chanzo chao. Hivyo inaelekea ni muhimu kwa Tanzania kwenda sambamba na hili pamoja na kujihakikishia utunzaji wa mazingira na usawa wa kiuchumi na kijamii/usawa wa kijinsia wa siku zijazo.

Kwa muhtasari wa hayo hapo juu, misukumo ifuatayo imebainishwa chini ya mkakati huu: Ongezeko la uzalishaji (1) mchakato wa uimarishwaji wa ubora wa masoko ya ndani na mazingira ya biashara (2), Kuongeza ubora (3) na uanzishaji wa masoko mapya, ukijumuisha masoko ya kahawa endelevu (4).

Kama mkakati huu wa kahawa ukitekelezwa, **unatarajiwa kuleta mapato ya ziada ya angalau Dola za Marekani M.150 kwa mwaka** (Dola za Marekani M.233 kwa bei ya sasa) katika uchumi wa kitaifa kupitia mapato ya nje. Kati ya jumla ya Dola za Marekani M.250 zinazozalishwa kwa mwaka na tasnia ya Kahawa (Dola za Marekani M.335 kwa bei ya sasa, angalau 75% ingegawanywa tena kwa wakulima wa Kahawa. **Hili lingekaribia kuongeza mara mbili (ongezeko la +95% ) mapato ya kahawa ya kadirio la kaya 400,000,** hivyo kuchangia kwenye kupunguza umaskini na kujenga uwezo endelevu na uboreshaji binafsi wa tasnia ya Kahawa.

## Utangulizi

### Mkakati uliotayarishwa kwa njia shirikishi na kuoanishwa na sera nyingine za kitaifa

Mkakati wa Maendeleo wa Tasnia ya Kahawa Tanzania 2011-2021 ni matokeo ya jitihada shirikishi za wadau wa tasnia hii. Mkakati huu unakuja kama mwendelezo wa maendeleo kadhaa ya hivi karibuni katika tasnia ya kahawa katika kipindi cha miaka michache iliyopita.

Mwaka 2009, Bunge liliridhia mabadiliko ya bodi za mazao ambazo hapo awali yalipendekezwa mwaka 2006. Hili lilisababisha "Marekebisho ya SHERIA YA BODI YA MAZAO NA. 23 ya mwaka 2009". Bodi ya Kahawa Tanzania ilikuwa imejiandaa kwa kuwa na uteuzi mpya wa Uongozi kushughulikia changamoto zilizotokana na mabadiliko ya Bodi za mazao (2008). Uongozi huu mpya ulianza kwa kutathmini ili kuchanganua hali ya Tasnia hii, na kubainisha vikwazo na mapungufu makubwa yanayosababisha kukwama kwa sekta hii. Mojawapo ya mahitimisho makuu lilikuwa ni haja ya uratibu wa mikutano ya Ubia wa Umma na Binafsi (PPP) katika kuyashughulikia "Majukumu shirikishi" katika sekta hii.

Hivyo, wadau walikaribishwa mwezi Desemba, 2009 kwenye Mkutano wa Kitaifa wa Kahawa (NCC) siyo tu kubadilishana taarifa, bali pia kujenga mwafaka katika dira ya pamoja ya siku za baadaye. Kwenye mkutano huu, miongoni mwa mambo mengine wadau waliamua kujenga Mkakati Mpya wa Maendeleo ya Tasnia 2011-2021 kwa kuzingatia SHERIA YA KAHAWA na majukumu shirikishi (PPP).

Mkakati huu ulianzishwa kupitia mashauriano ya wanachama wote wa mnyororo wa thamani (wakulima, ushirika/wanunuzi, wasindikaji, wasafirishaji, watafiti,watoa huduma za ugani, Mamlaka ya Serikali za Mitaa, Serikali, Bodi ya Kahawa Tanzania, vyama vinavyowakilisha sekta binafsi). Mikutano ilifanyika katika mikoa mikuu ya uzalishaji kujadili masuala yaliyopo na kukubaliana kuhusu vipaumbele: Arusha, Manyara, Kilimanjaro, Iringa, Mbeya, Kagera, Kigoma na Ruvuma. (Muhtasari na mapendekezo yatatolewa chini ya kiambatisho cha 3). Mikutano hii ilihudhuriwa na wadau 600 kutoka wilaya 28. Mkakati huu uliridhiwa na zaidi ya wawakilishi 120 wa tasnia hii wakati wa Mkutano wa Kitaifa wa Kahawa, tarehe 27, Mei, 2011. Toleo hili la sasa lililofanyiwa marekebisho, pamoja na kujumuishwa katika mpango wa utekelezaji lilithibitishwa mwezi wa Aprili, 2012.

Waraka huu unaanzisha mkakati wa kuiboresha tasnia hii na hivyo, kujenga tasnia ya Kahawa Tanzania iliyo endelevu na yenye faida kwa wadau wote. Kiini cha mkakati huu ni kuboresha mapato na riziki ya wakulima wa Kahawa Tanzania na kuboresha tasnia kwa kuongeza wingi na ubora wa Kahawa inayozalishwa nchini Tanzania.

Mkakati huu unalenga kufungamana na sera/jitihada za kitaifa, kama vile:

1) Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (MKUKUTA)
2) Mkakati wa Maendeleo ya Sekta ya Kilimo (ASDS) na Mpango wa Maendeleo ya Sekta ya Kilimo (ASDP) na;
3) 'Kilimo Kwanza' kinacholenga kuongeza uzalishaji katika kilimo Tanzania kote.

# 1. Muktadha wa jumla wa Sekta ya Kahawa Tanzania

Mkakati huu ulianzishwa kwa kuzingatia kuwepo kwa fursa za masoko ya Kimataifa na kwa kuzingatia hali ya sasa ya tasnia ya Kahawa Tanzania pamoja na matatizo makubwa yanayoikabili tasnia hii.

## 1.1 Fursa ya Tasnia ya Kahawa Tanzania katika Masoko ya Dunia

Kahawa ni chanzo muhimu cha mapato kwa nchi nyingi, ikiwemo Tanzania. Huchangia karibu Dola za Marekani bilioni 16.5 katika uchumi wa dunia (2010). Hivi sasa uzalishaji wa kahawa duniani unakadiriwa kufikia zaidi ya magunia milioni 130 ya kg 60. Brazil na Vietnam zinaongoza katika uzalishaji na kwa pamoja huwakilisha kiasi pungufu kidogo ya nusu ya kahawa yote duniani. Afrika huchangia kiasi cha 12% cha kahawa yote duniani; hisa ya Tanzania ni chini ya asilimia moja ya uzalishaji wote duniani (0.6% katika mwaka 2011).

Kimsingi, biashara ya Kahawa duniani inatawaliwa na aina mbili za kahawa, Arabika na Robusta. Arabika huwakilisha karibu 60% ya kahawa yote inayosafirishwa nje (karibu nusu ya hii ni ya asilia, na nusu nyingine ni Arabika laini) ambapo Robusta huwakilisha karibu 40% ya kahawa yote inayosafirishwa nje.

Kwa kuzingatia mielekeo ifuatayo katika masoko ya kahawa ya Kimataifa tasnia ya kahawa ya Tanzania ina fursa kubwa kwa maendeleo ya siku za baadaye.

### 1.1.1 Ukuaji endelevu wa uhitaji wa kahawa duniani, hususan kuhusu masoko yanayoibuka

Ongezeko katika matumizi ya Kahawa limekuwa thabiti kwa wastani wa kiasi cha 1.5% hadi 2% kwa mwaka katika miongo kadhaa iliyopita. Kushuka kwa uchumi na migogoro ya kiuchumi haikuwa na matokeo mabaya kwenye punguzo hili linaloongezeka, kimsingi shukurani nyingi kwa nchi zilizopiga hatua za haraka za maendeleo ya matumizi ya kahawa katika nchi zinazoibukia na kuzalisha kahawa (Brazil, China, India, Ulaya ya Mashariki, n.k.) Kinyume chake, kumekuwepo na ongezeko dogo katika uhitaji kutoka masoko ya asili (Ulaya, Marekani, Japan). Hili linaelekea kuonyesha mabadiliko endelevu katika jiografia ya biashara ya kahawa, ambayo yangekuwa na uwezekano wa kuongoza nchi zinazozalisha kama Tanzania ili kutia moyo zaidi utangazaji wa kahawa yao kwenye masoko mapya.

Wakati huohuo, uwezekano wa uzalishaji katika ngazi ya dunia (husuan Brazil na Vietnam) unapatiwa ukomo na ukuaji wa miji, ushindani kutokana na mazao mengine, na uhamiaji katika shughuli nyingine za kiuchumi. Kuna uwezekano, unaohusishwa na changanuzi kadhaa za Shirika la Kimataifa la Kahawa (1CO) kwamba maendeleo katika ukuaji wa mahitaji hayatakidhiwa kikamilifu na nchi asilia, hivyo kufungua fursa ya wazalishaji wengine waliopo katika maeneo ambayo hayajaendelezwa, kama vile Tanzania ili kuongeza uzalishaji.

### 1.1.2 Uendelezaji wa masoko, vishubaka "kahawa mahususi" kwenye kiwango cha Kimataifa

Miaka 10 iliyopita imeshuhudia maendeleo ya haraka ya masoko maalumu kwa kahawa ya ubora wa hali ya juu kabisa katika masoko ya walaji (Marekani, Japan, Ulaya, nchi zinazoibuka). Hili limechochewa na ongezeko la wingi wa maduka ya kahawa, pamoja na ongezeko la haraka la matumizi ya kapsuli ya kahawa inayootumiwa mara moja nyumbani. Mara nyingi kahawa hii huitwa "kahawa mahususi' au "kahawa ya gourmet" ingawa hakuna maainisho yaliyokubalika kwa istilahi hizi. Kutokana na kiwango halisi cha ukuaji cha sekta hizi pamoja na hisa ya soko la sasa ni vigumu kuelezea. Hata hivyo, kimsingi kahawa mahususi hufikiriwa kuchangia kiasi cha 10% ya matumizi duniani (ITC, The Coffee Exporter's Guide).

Arabika laini ya Tanzania ni maarufu kwa asidi yake,mng'ao na sifa yake iliyojaa ladha na hunufaika kutokana na mtazamo chanya kuhusu mandhari ya kimataifa. Kwa ujumla, wataalamu huifikiria kwamba ni ya ubora sawa na ya nchi jirani ya Kenya, hata hivyo, wakati mwingine inaweza kukosa uthabiti. Kahawa ya Piberi kutoka Mlima Kilimanjaro na Mlima Meru pia imevutia katika soko la Marekani la kahawa mahususi ikiuzwa kwa bei ya thamani ya juu.

Tanzania inaweza kunufaika kutokana na ubora wa uwezo huu wa kahawa uliotukuka kuweka hisa ya ongezeko la uzalishaji wake kwenye umahususi wa masoko ya vishubaka. Kihistoria masoko ya kahawa yamekua na kubadilika kwa haraka kutokana na kuitegemea mno Brazil kama mzalishaji (baridi ya kuikiza, ukame, viwango vya ubadilishaji wa fedha, n.k), pamoja na athari za uvumi unaoyumbisha fedha. Tafiti za hivi karibuni zimedhihirisha kwamba masoko ya kahawa mahususi kwa ajili ya kahawa ya ubora wa hali ya juu kabisa ina uwezekano mdogo zaidi wa wepesi wa kubadilika. Ingawa kwa hakika siyo suluhisho kamili, sehemu ya kahawa mahususi, huwapatia wakulima wa kahawa fursa yenye msisimuko.

### 1.1.3 Ongezeko la umuhimu wa masuala endelevu na miongozo ya uwajibikaji wa kijamii – kimazingira (uthibitisho, uhakikisho, kanuni za maadili)

Pamoja na vipengele vya ubora, tasnia ya kahawa dunia inakua kwa haraka kuelekea viwango endelevu (oganiki, FLO, UTZ, 4C Rainforest, n.k), hususan katika sehemu za thamani mahususi: Ukubalifu wa viwango hivi unaweza kutoa fursa kwa thamani za juu na unaweza kuzidi kuwa hitaji la muhimu katika tasnia hii.

Kama mfano, mpango uliothibitishwa na UTZ ulitaarifu kwamba waliona ongezeko la +49% la kahawa iliyothibitishwa mwaka 2010 na kwamba hisa yao ya soko katika nchi ya Uholanzi na Uswisi hivi sasa inafikia 40%. Ingawa sekta hii inakua haraka, lakini ukubwa wa uwezo wake wa soko katika ngazi ya dunia una haja ya kulinganishwa. Hata ukifikiriwa kama mpango mkubwa kabisa endelevu wa kahawa ambao UTZ umepata kuthibitisha, huwakilisha kiasi cha 1.5% ya uzalishaji wa dunia.

Wakulima wa kahawa wa Tanzania watahitaji kushawishiwa kwamba kwao inawezekana kujihakikishia mavuno mengi yenye faida wakati wakizingatia viwango vya aina hiyo. Hivyo basi, ingeweza kuwa njozi kuitegemea tasnia ya kahawa Tanzania kubadilika kabisa na kuingia katika viwango endelevu katika kipindi cha

miaka michache. Jitihada kadhaa zinadhihirisha faida zitakazopatikana kutokana na matumizi ya viwango vya uendelevu: Matumizi endelevu ya Kanuni Bora za Kilimo (GAP), na Kanuni bora za Usimamizi (GMP) zingeweza kusaidia uhifadhi wa mazingira kwa ajili ya vizazi vijavyo, usawa wa kiuchumi na kijamii, pamoja na uibukaji wa mifumo fanisi ya kilimo itakayosababisha uzalisahaji bora zaidi.

### 1.1.4 Faida za kiushindani zinazotarajiwa kwa Tanzania katika masoko ya kahawa ya kimataifa

Kimsingi, Tanzania huzalisha aina tatu za kahawa: Arabika laini iliyooshwa (kiasi cha 55% ya jumla ya kahawa inayozalishwa), Robusta inayokaushwa kwa jua (kiasi cha 40% ya kahawa inayozalishwa), pamoja na kiasi kidogo cha Robusta ya asili inayokaushwa kwa jua (chini ya 5% ya kahawa yote inayozalishwa). Zaidi ya 90% ya kahawa inayozalishwa husafirishwa na kuuzwa kwenye soko la kimataifa. Kiasi cha Kahawa inayosafirishwa nje imekuwa ni kati ya magunia 600,000 na 950,000 kwa miongo miwili iliyopita. Wanunuzi wakubwa katika soko la dunia ni Japan (kiasi cha 30% ya thamani ya mauzo ya nje), ikifuatiliwa na Marekani (kiasi cha 15% ya thamani ya mauzo ya nje), halafu Ujerumani, Italia na Ubelgiji (takriban 10% ya thamani ya mauzo ya nje kwa kila nchi). Asilimia 25 iliyosalia inagawanywa miongoni mwa nchi nyingi tofautitofauti kutoka Finland hadi Swaziland. Jumla ya thamani ya mauzo ya nje ilifikia kiasi cha Dola za Marekani milioni 145 mwaka 2011 (ITC COMTRADE).

Katika muktadha huu Tanzania inanufaika na faida kadhaa za kiushindani ambazo zingeweza kuendelezwa zaidi katika miaka ijayo.

<u>Faida ya kiushindani inayotarajiwa kwa washindani wa Amerika ya Kati kuhusu soko la Arabika laini</u>

Tanzania ni mzalishaji wa “Arabika laini ya Kolombia”. Kahawa ya Kolombia laini ina jumla ya 9% ya uzalishaji wa dunia. Hata hivyo inachukuliwa kwamba buni hiyo ya ubora wa juu inatawala kwa bei bora kabisa kwenye masoko ya Kimataifa. Kolombia na Kenya ndio wazalishaji wengine pekee wa ubora huu. Tanzania hutoa kiasi cha 6% ya uzalishaji wa kundi la Kolombia laini. Washidani wengine ni pamoja na kundi la “Kahawa laini nyingine” lililotawaliwa na nchi za Amerika ya Kati. Japani na Ujerumani zinawakilisha maeneo mawili makuu ya ununuzi wa kahawa ya Arabika laini inayotoka Tanzania. Kwa pamoja zinachangia kiasi cha 60% na 70% ya mauzo ya nje ya kahawa ya Arabika wakati hisa za masoko mapya, kama vile Marekani, Italia na Ubeligiji zinaonekana kuongezeka. **Tanzania ina uwezo wa kinadharia wa kuuza nje Arabika laini mapema kuanzia Julai/Agosti, mbele ya majira ya Amerika ya Kati, wakati ambapo soko la dunia lina upungufu wa Arabika mpya yenye ubora.** Kuna fursa kubwa kwa tasnia ya kitaifa kuitumia nafasi hii kupata bei za juu ili mradi mda wa sasa unaohitajika kusafirisha kahawa nje unapunguzwa. Masuala ya usafirishaji wa sasa, mchakato wa uuzaji na vikwazo vya kiutawala havina budi kuzingatiwa kama vikwazo vya dhati katika suala hilo.

Nafasi ya kipekee kwa masoko ya Japan – Shukurani kwa mvuto wa kahawa ya "Kilimanjaro"

"Tanzania inanufaika kwa kupata nafasi ya kipekee nchini Japan – shukurani kwa kuwepo kwa mvuto wa "Kilimanjaro". Kwa mujibu wa utafiti wa hivi karibuni kutoka PROMAR,

> *" Kilimanjaro" ni aina ya Kahawa inayotambulika na kupendwa sana katika masoko ya Japani; na neno "Kilimanjaro" lina nguvu ya uuzaji.*

Ambapo mwanzoni ilitambulika kama Kahawa laini ya Arabika kutoka Mkoa wa Kilimanjaro uliopo Tanzania, Baraza la Maonyesho ya Biashara Japan liliamua kwamba Kahawa yote ya Arabika laini inayozalishwa nchini Tanzania ingeweza kuwekewa alama ya Kahawa ya "Kilimanjaro" bila kujali iwapo inazalishwa Kilimanjaro au katika Nyanda za Juu Kusini (1991). Aidha, aina ya kahawa yenye 30% au zaidi ya kahawa laini za Arabika pia inaweza kuwekewa lebo ya "Kilimanjaro". Uamuzi huu pia ulimaanisha kwamba kahawa iliyozalishwa katika nchi nyingine za Kiafrika haingeweza kuuzwa Japan kwa lebo ya "Kilimanjaro. Hili limechangia sana kwenye ongezeko la mauzo ya nje ya kahawa ya Tanzania kuelekea Japan katika miaka ishirini iliyopita.


Tasnia ya kahawa nchini Tanzania ingeweza kufikiria idadi kadhaa za jitihada ili kuzidisha nafasi hii ya kipekee kwenye soko la Japan, ikiwa ni pamoja na makubaliano ya ubia wa moja kwa moja, Kampeni za matangazo , n.k.

## 1.2 Hali ya Kahawa ya Tanzania

### 1.2.1 Umuhimu wa sekta ya Kahawa

Kahawa ni mojawapo ya mazao makuu yanayouzwa nchi za nje, ambayo inachangia kiasi cha 5% ya thamani ya jumla ya mauzo ya nje, 24% ya mazao ya asili na inazalisha mapato ya wastani wa Dola za Marekani milioni 100 kwa mwaka kwa zaidi ya miaka 30. Tasnia hii hutoa mapato ya moja kwa moja kwa zaidi ya kaya za wakulima 400,000 hivyo, kusaidia utafutaji riziki ya Watanzania milioni 2.4.

**Jedwali la 1: Kahawa kama inavyoonekana miongoni mwa mazao ya asili yanayouzwa nje (asilimia ya jumla ya thamani ya mazao ya asili yanayouzwa nje)**





Chanzo: Ripoti ya uchumi ya mwezi, Benki ya Tanzania, 2011

### 1.2.2 Mabadiliko makubwa katika tarakimu za uzalishaji kwa miongo iliyopita

Viwango vya uzalishaji vilivyopo havitofautiani sana kwa wastani wa uzalishaji wa mwaka wa tani 50,000 uliowekewa kumbukumbu katika miaka 30 iliyopita (1980-2010). Tokea zamani, uzalishaji umekuwa ukipanda na kushuka kiwango cha chini kikiwa ni tani 33,000 na cha juu tani 68,000. Takribani asilimia 90% ya kahawa inayozalishwa Tanzania huuzwa kwenye masoko ya nje.

**Jedwali la 2: Makadirio ya mabadiliko ya uzalishaji/uuzaji nje wa Kahawa (1971-2011)**





**Chanzo: Takwimu za USDA 2011**

Wakati takwimu za uzalishaji zikionekana kutobadilika sana, mabadiliko makubwa yametokea kwenye mkusanyiko na chanzo cha uzalishaji wa kahawa ya Tanzania.

- Kiasi cha uzalishaji wa kahawa ya Robusta kimeongezeka mara mbili katika kipindi cha miaka thelathini iliyopita.


- Kwa upande waArabika laini, uzalishaji katika eneo la Kaskazini (Kilimanjaro, Arusha, Manyara na Tanga), umeshuka sana, ambapo maeneo ya Kusini (Mbeya na Mbinga) kumekuwepo na ongezeko kubwa. Kumekuwepo na mabadiliko machache ya uzalishaji wa Arabika ngumu ya asili (maeneo ya Tarime).

**Jedwali la 3: Mabadiliko katika viwango vya uzalishaji wa kahawa ya Arabika na Robusta kwenye uzalishaji kwa ujumla katika Tanzania (1980-2011)**




Chanzo: Takwimu za Bodi ya Kahawa Tanzania 2011

**Jedwali la 4: Mabadiliko ya mchango wa uzalishaji wa kahawa ya Arabika kutoka kwenye kila eneo la uzalishaji kulinganisha na kahawa inayouzwa nje ya nchi (1980-2008)**




Chanzo: Takwimu Bodi ya Kahawa Tanzania 2009

### 1.2.3 Maeneo ya uzalishaji na sifa zake

Tanzania imejaliwa ardhi tele yenye mwinuko, hali joto, mvua na udongo vinavyofaa kwa uzalishaji wa kahawa aina ya Arabika na Robusta zenye ubora wa hali ya juu. Mikoa mikuu ya uzalishaji wa kahawa aina ya Arabika ni Kilimanjaro, Arusha, Mbeya na Mbinga/Ruvuma. Robusta huzalishwa hasa katika Mkoa wa Kagera. Mikoa mingine ya uzalishaji ni pamoja na Tanga, Iringa, Morogoro, Kigoma, Manyara, Mwanza, Rukwa na Mara.

Nchini kote, kahawa huzalishwa katika mifumo mikuu mitatu ya uzalishaji:

- Kahawa hulimwa pekee bila kuchanganya na mazao mengine/wakulima wadogo wadogo (hasa maeneo ya Kusini)
- Kahawa huchanganywa na migomba/wakulima wadogowadogo (hasa maeneo ya Kaskazini na Magharibi)
  Hulimwa kwenye mashamba makubwa (chini ya 10% ya uzalishaji wa kahawa yote nchini)

Maelezo mafupi ya hali halisi katika kila eneo la uzalishaji yametolewa hapa chini.

**Ukanda wa Kaskazini (Kilimanjaro, Arusha, Manyara, Tanga)**

Ukanda huu huzalisha aina ya kahawa laini ya Arabika ambayo ni nzuri kabisa duniani kote. Eneo linalolimwa kahawa linakadiriwa kufikia hekta 83,000 likiwa na uzalishaji wa wastani wa kiasi cha tani 7,500 hadi tani 10,000 za kahawa kavu kwa mwaka. Mfumo wa uzalishaji ni mchanganyiko kati ya wakulima wadogo ambao ni wengi (ambao huchanganya migomba na kahawa) na mashamba makubwa machache ambayo zaidi yako katika Mkoa wa Arusha.

Uwezo/Sifa za kipekee*:*

\+ Uwezo wa kuzalisha kahawa yenye ubora wa hali ya juu unaotambuliwa Kimataifa
\+ Uzalishaji wa kahawa wa asili wa muda mrefu na utaalamu wa hali ya juu
\+ Upatikanaji wa huduma za usindikaji, viwanda vyaukoboaji na miundombinu mizuri ya usafirishaji n.k
\+ Uwezekano wa ukarabati wa mitambo ya kati ya kumenyea kahawa (CPUs) ambayo iko kwenye hali mbaya

- Mibuni mingi imezeeka
- Uzalishaji ni mdogo sana: kiasi cha kilo 100-125 za kahawa safi kwa hekta
- Ushindani kutokana na mazao mengine (eneo linafaa kwa uzalishaji wa aina za mazao mbalimbali ya kilimo na wakulima kukata tamaa na kuamua kung'oa kahawa)

**Wilaya ya Mbinga, Ruvuma katika Nyanda za Juu za Kusini mwa Tanzania**

Hapo zamani eneo lilikuwa likizalisha kahawa ya biashara aina ya "Amex". Hivi sasa eneo hili ni miongoni mwa maeneo nchini yanayozalisha kahawa za Arabika laini ambazo ni bora. Kiasi cha 70% ya uchumi wa wilaya ya Mbinga hutegemea uzalishaji wa kahawa ambao unafikia tani takriban 10,000 kwa mwaka. Eneo linalo limwa kahawa linakadiriwa kuwa hekta 35,000 na ardhi iliyopo inaruhusu upanuzi zaidi. Wilaya inapata milimita 1,000 hadi 2,000 za mvua kwa mwaka, hivyo kuifanya iwe na hali nzuri ya hewa kwa uzalishaji wa kahawa ya ubora wa hali ya juu.

Uwezo/*Sifa za kipekee:*

\+ Ubora wa hali ya juu
\+ Kuongezeka kwa idadi ya mitambo ya kati ya kumenyea kahawa (CPUs)
\+ Uzalishaji wa kahawa gredi ya 18 (Screen 18)

- Ukosefu wa vyanzo vya fedha (mitaji)

- Ukosefu wa miche ya aina bora na pembejeo zilizohakikiwa

**Mkoa wa Mbeya**

Mkoa wa mbeya umejitokeza kuwa mkoa wa kwanza unaozalisha Arabika laini inayokadiriwa kuwa tani 12,000 hadi 15,000 kwa mwaka. Mbeya ni mkoa unaopanuka katika uzalishaji wa kahawa, ukiwa na kiasi cha hekta 51,000 zinazozalisha kahawa na idadi ya mitambo ya kati ya kumenya kahawa inaendelea kuongezeka.

*Uwezo/Sifa za kipekee:*

+ Kuongezeka kwa idadi ya CPU
+ Uwepo wa miradi endelevu (UTZ, Oganiki, n.k)

- Ukosefu wa vyanzo vya fedha(mitaji)
- Ukosefu wa miche ya aina bora na pembejeo zilizohakikiwa

**Eneo la Kagera**

Eneo hili linajumuisha Wilaya za Muleba, Karagwe, Misenyi na Bukoba ambazo kimsingi huzalisha kahawa aina ya Robusta. Eneo hili linakadiriwa kuzalisha tani 21,000 za Kahawa safi kwa mwaka katika eneo lipatalo hekta 51,000. Wastani wa uzalishaji ni kg 500 ya kahawa safi kwa hekta.

*Uwezo/Sifa za kipekee*

+ Uwezo wa kuzalisha kahawa yenye ubora wa hali ya juu
+ Ukaribu na nchi ya Uganda
+ Uwezekano wa kufanya majaribio kwa ajili ya uzalishaji wa Kahawa ya Robusta iliyooshwa (matumizi ya CPU zinazotumia maji kidogo hasa ikitiliwa maanani ugumu wa upatikanaji wa maji)

- Madhara ya ugonjwa wa mnyauko fuzari (CWD) na umuhimu wa kupanda aina ya miche bora yenye ukinzani dhidi ya ugonjwa wa mnyauko fuzari
- Kanuni zirekebishwe ili kuruhusu biashara halali na yenye ufanisi na nchi ya Uganda

**Eneo la Tarime**

Tarime ina sifa ya kuzalisha Kahawa ya Arabika Ngumu inayosindikwa kwa njia asilia ya kukausha. Wilaya inakadiriwa kuzalisha chini ya tani 1,000 za kahawa safi kwa mwaka katika eneo la hekta 2,900. Kuna wakulima wapatao 8,000. Eneo la Tarime hupata mvua mara mbili kwa mwaka kiasi cha milimilita 1200 hadi 1600 katika sehemu za miinuko (nyanda za juu) na milimita 900-1200 katika maeneo ya kati (nyanda za kati).

*Uwezo/Sifa za kipekee:*

+ Ubora ambao wakati mwingine hulinganishwa na kahawa ya Sidamo iliyokaushwa kwa jua
+ Uzalishaji unaweza kuongezeka kwa kuongeza hekta 35,000 za ziada (TaCRI)

- Ugumu wa ukusanyaji kahawa na usafirishaji wakati wa majira ya mvua

- Uzalishaji mdogo
- Kutofahamika (Haijulikani kwenye masoko ya Kimataifa)


**Eneo la Kigoma**

Uzalishaji wa kahawa katika mkoa wa Kigoma uko katika hatua za mwanzo,na huzalishwa na familia takriban 4,000. Uzalishaji wa kahawa mkoani Kigoma bado uko chini, kiasi cha tani 1,000 kwa mwaka kwenye eneo linalokadiriwa kuwa hekta 6,600.

**Uwezo/Sifa za kipekee:**

+Ubora wa hali ya juu sana (ilishinda Tuzo ya "Taste of Harvest award for East, South and Sub-Sahara Africa")
+ Uwepo wa maeneo yanayofaa kwa uzalishaji wa kahawa yenye ubora wa hali ya juu na maeneo kwa ajili ya upanuzi
+ Kuwa karibu na nchi za Burundi, Jamhuri ya Kongo, Rwanda (kuwa ufukweni mwa Ziwa Tanganyika)
- Eneo limejitenga sana hivyo kuwepo na ugumu wa usafiri (barabara, reli n.k)
- Kiasi kidogo cha uzalishaji (Kahawa imeanza kulimwa hivi karibuni katika eneo hili), hivyo kuna wadau wachache katika tasnia ya kahawa eneo hilo.

**Kielelezo cha 5: Ramani ya Maeneo Makuu ya Uzalishaji wa Kahawa nchini Tanzania**




Chanzo: KPN

## 1.3 Changamoto kuu zinazoikabili tasnia ya Kahawa nchini Tanzania

Tasnia ya kahawa nchini Tanzania inakabiliwa na changamoto mbalimbali, ikiwa ni pamoja na tija ndogo, bei ndogo za shambani zinazosababishwa na mfumo wa masoko ya ndani/mazingira ya biashara kutofanyakazi kwa ufanisi, kutotumika ipasavyo kwa fursa za ubora pamoja na tishio la mabadiliko ya tabia nchi.

### 1.3.1 Uzalishaji mdogo na faida za kiuchumi za mashamba ya kahawa

Uzalishaji kahawa uliodumaa nchini Tanzania, kwa kiasi kikubwa, ni matokeo ya kupungua kwa mavuno. Mojawapo ya sababu kuu za tatizo hili ni kuwepo kwa mibuni iliyozeeka pamoja na kutozingatia kanuni bora za kilimo cha kahawa. Kwa kawaida inafahamika kuwa, mbuni hauna

faida kiuchumi unapozidi  umri wa miaka 20-25.  Nchini Tanzania, kiasi kikubwa cha mibuni ipatayo  milioni 240 imevuka umri huu (Friedrich Erbert Stiftung 2004). Hivyo basi, uzalishaji wake umekuwa ukipungua taratibu katika kipindi cha miaka mingi, ukizidi kuendelea kupunguza uzalishaji kitaifa.  Kwa ujumla, hali hii imesababishwa  na utunzaji mbaya wa mashamba ikiwa ni pamoja na kutokupogoa, kurengeta, udhibiti mbaya wa wadudu waharibifu na magonjwa hususan mnyauko fuzari (CWD) katika maeneo ya Robusta,na chulebuni (CBD) na kutu ya majani (CLR) katika maeneo ya Arabika.Ingawa, kwa kiasi fulani, mibuni mipya imepandwa maeneo ya Kusini (wastani wa umri wa mibuni ni kama miaka 25), lakini sehemu kubwa ya Kaskazini na hususan Mkoa wa Kilimanjaro, inaathiriwa  na tatizo hili (wastani wa umri wa mibuni ni zaidi ya miaka 40).  Katika maeneo haya, tatizo hili linachangiwa zaidi na  upandaji mbaya wa migomba na mazao mengine ambayo husababisha upungufu wa rutuba na kuongezeka kwa kivuli .

Kukosekana kwa upandaji mpya, kwa kiasi kikubwa ni matokeo ya kuwepo kwa huduma za ugani zisizo tosheleza hususan kwenye masuala ya agronomia ya  kilimo cha kahawa.  Hadi mwanzoni mwa miaka ya 1980, huduma za ugani zilikuwa zikitolewa na Bodi ya Kahawa Tanzania.  Hivi sasa huduma hizi ziko chini ya Serikali za Mitaa ambazo hutoa huduma za ugani kwa  mazao yote.  Ubora wa huduma hizi hutofautiana kutoka eneo moja hadi eneo jingine, lakini mara nyingi hakuna wataalamu wa kutosha na wakati mwingine wataalamu hawana utaalamu mahususi wa kilimo cha kahawa.  Hili linaweza kusababisha matumizi yasiyo sahihi ya pembejeo na hatimaye husababisha hasara kubwa kutokana na wadudu waharibifu na magonjwa.  Hili ni mojawapo ya vikwazo  dhidi ya juhudi zozote zinazolenga ufufuaji wa kiasi kikubwa cha mibuni nchini kote. Juhudi zozote kubwa za kupanda tena  aina bora ya mibuni ni muhimu kwa kuwa itasaidia kupunguza gharama za uzalishaji (punguzo la matumizi ya pembejeo, viuatilifu, viuakuvu) huku zikiongeza mavuno na kuruhusu kilimo cha kahawa kuwa cha faida kiuchumi.

Tatizo lingine kubwa ni ugumu wa kupata pembejeo, pembejeo za ubora halisi (mbolea za chumvichumvi, viuatilifu, viuakuvu).  Upandaji mkubwa wa mashamba ya kahawa kwa kutumia aina bora utaweza kusaidia kupunguza kiasi kikubwa cha pembejeo kinachohitajika ikiwa ni pamoja na kuongezeka kwa kipato cha wakulima hivyo kuongeza uwezo wa kifedha na kukidhi mahitaji.

### 1.3.2 Bei za chini za shambani ni matokeo ya  kutofanyakazi kwa ufanisi wa hali ya juu wa soko la ndani na gharama kubwa za kibiashara

Kwa mujibu wa utafiti wa hivi karibuni (Coles na Mhando) baadhi  ya wakulima wa kahawa wa Tanzania wanaweza kupata kiasi kidogo hadi 50% ya bei ya mnada kwa kahawa wanayoizalisha.Kwa ujumla zaidi, inakadiriwa kwamba wakulima wa kahawa hupata wastani wa 65% hadi 70%  wa bei ya FOB.  Matokeo ya wakulima kupata kiwango hiki kidogo cha kipato, ni kwamba kilimo cha zao la kahawa kwa  sasa sio shughuli inayoleta faida  kiuchumi.  Hivyo, wakulima hawana motisha ya kuwekeza muda au mtaji ili kuongeza uzalishaji na ubora.

**Hali hii ni mchanganyiko wa muingiliano wa sababu mbalimbali:**

- Ucheleweshaji dhahiri unaosababishwa na mfumo wa soko la ndani na mazingira ya biashara (inakadiriwa kwamba kiasi cha miezi mitatu (3) inahitajika kuhamisha kahawa kutoka shambani hadi bandarini-FOB).
- Taarifa za soko zisizotosheleza na uwazi
- Gharama za juu za usafirishaji wa ndani/kodi za ndani
- Utendaji duni wa vyama vya ushirika

Mfumo wa mnada unaonekana kuwa na faida nyingi, ikiwa ni pamoja na bei nzuri katika mnyororo wa thamani pamoja na udhibiti wa bidhaa zinazouzwa nje. Katika mfumo wa sasa pia inaweza kujumuisha ucheleweshaji wakati kahawa inapo nunuliwa kutoka kwa mzalishaji (bei ya shambani) na wakati pale inapouzwa mnadani na kulipiwa. Muda huu mrefu hujenga mazingira hatari ya bei kwa mnunuzi wa kahawa (ushirika au binafsi) kwa sababu ya kubadilikabadilika kwa bei za kimataifa pamoja na kutokuwa na uhakika kuhusu bei ya mwisho na uwezekano wa kupata bei ya nyongeza inayoweza kutokana na minada. Matokeo yake, wanunuzi wa kahawa wanaelekea kusimamia hatari za bei kwa kutoa bei ndogo za shambani ambazo sio wakati wote zinafidiwa kwa malipo ya pili pale ambapo bei ya mwisho ni nzuri.

Wakati mwingine, ukosefu wa taarifa za masoko huwazuia wakulima wa kahawa kuwa na dira dhahiri juu ya bei halisi wanayotakiwa kupata kutokana na mazao yao. Hii ni dhahiri katika maeneo ambako hakuna ushindani wa kutosha miongoni mwa wanunuzi wa ndani/vyama vya ushirika.

Gharama kubwa za usafirishaji huathiri sana bei ambazo wakulima huzipokea pamoja na tija (tatizo la upatikanaji wa pembejeo). Kwa kiasi kikubwa haya ni matokeo ya miundombinu ya usafiri kuwa haitoshelezi, barabara kutopitika wakati wa msimu wa mvua, na barabara mbovu. Maeneo ya uzalishaji kahawa Tanzania yanajumuisha eneo kubwa la ardhi. Hili linahitaji kuwa na miundombinu au mtandao wa barabara na reli ambao unahakikisha kwamba kahawa inasafirishwa kwa ufanisi na kwa gharama nafuu. Nchi imeshuhudia uboreshaji mkubwa katika hali za barabara katika miaka michache iliyopita, ikiwa ni pamoja na barabara kuu za lami kati ya Dar es Salam na Mtwara na Dar es Salaam na Lindi. Katika mfumo huohuo, bandari ya Dar es Salaam imeboreshwa ingawa bado ina tatizo la msongamano.

Vikwazo vya kimiundombinu si vikwazo pekee. Mambo mengine ni pamoja na vikwazo vya usafirishaji, ukosefu wa maghala ya kutosha na matatizo ya usimamizi wa mikataba. Kodi za ndani na matatizo mengine ya kiutawala pia huchangia kuongezeka kwa gharama za kibiashara na hivyo kupunguza bei za shambani.

Mwisho, kuna baadhi ya matukio ya ushirika yanayoongeza gharama zisizo za lazima za uendeshaji kwa wakulima na hivyo kupunguza bei ya shambani kwa sababu ya usimamizi au uongozi hafifu.

### 1.3.3 Ubora wa hali ya juu usiopewa kipaumbele

Inakadiriwa kwamba kiasi cha 90% ya Kahawa ya Tanzania kinasindikwa nyumbani (Hans R. Neumann Stifting) na hivyo kusababisha ubora usio thabiti kwa sababu ya kutofuata kanuni bora za usindikaji. Kwa hiyo wanunuzi wakubwa wa kimataifa hivi sasa hupendelea kutumia kahawa ya Tanzania ili kuongezea ladha kwenye kahawa nyingine badala ya kuendeleza kahawa ya Tanzania kama kahawa yenye asili ya kipekee.

Awali imedhihirika kuwa (Sura ya 1.1) Tanzania ina uwezo wa faida ya kiushindani kwenye soko la Kimataifa – shukurani kwa uwezo wake wa ubora. Kwa vipengele vingi, kwa ujumla ubora wa kahawa ya Tanzania ni mzuri kwa wastani kama inavyojidhihirisha katika bei za kahawa. Hata hivyo, hii haimaanishi kutokuwepo kwa mielekeo kadhaa ya mgongano:

- Vikwazo vya agronomia, kama vile matumizi madogo ya pembejeo, kutozingatia kanuni bora za kilimo kunasababisha kupungua uwiano wa madaraja ya juu (rejea takwimu kuhusu madaraja ya kahawa) hususan katika maeneo ya uzalishaji ya Kaskazini.
- Kuhusu usindikaji mdogomdogo wa Arabika laini, ukosefu wa maji safi ni tatizo kubwa katika baadhi ya maeneo ya uzalishaji, pamoja na idadi isiyotosheleza ya mashine za kumenyea kahawa na meza za kukaushia. Hili limesababisha kushuka kwa kiasi kikubwa kwa ubora katika miaka kadhaa, (sifa ya ladha/uchachu)
- Kuhusu usindikaji wa Arabika laini kwenye CPU, kuna idadi isiyotosheleza ya CPU zinazofanya kazi, hususan eneo la Kaskazini na baadhi yake zinakabiliwa na matatizo ya usimamizi na uendeshaji (ukusanyaji wa kahawa mbivu, upangaji bei, idadi isiyotosheleza ya meza za kukaushia).
- Kuhusu Robusta (eneo la Kagera) kwa ujumla huzalishwa kwa kukausha kwa jua na ina ubora wa wastani. Inasemekana kuwa kulikuwepo na mpango wa kuanzisha vituo vya kuzalisha Robusta iliyooshwa lakini tatizo la upatikanaji wa maji na nyongeza ya bei ambazo zingeweza kupatikana bado hazijadhihirishwa bayana.

Kwa kuzingatia uhaba wa maji nchini kote, na umuhimu wa kuzingatia mabadiliko ya tabia nchi, inapendekezwa kutumia teknolojia ya kisasa kabisa ya kiikolojia ya kuoshea kahawa kwenye mitambo ya kuondoa utelezi yenyewe kila inapowezekana. Mashine hizi za kiikolojia za aina hiyo za kuoshea kahawa zinatambulika kwa kutumia 10% tu ya maji ambayo kwa kawaida hutumiwa na CPU za kawadida.

Mwisho, ifahamike kwamba kahawa inayozalishwa kwa kukaushwa na jua au iliyozalishwa kwa mashine za mkono si lazima iwe ni ya kiwango cha chini cha ubora kuliko iliyozalishwa kwa CPU ili mradi imefuata masharti ya utayarishaji. Hata hivyo, usimamizi wa usindikaji huu ni mgumu zaidi na huhitaji umakini na uzingatiaji wa kanuni bora.

### 1.3.4 Matokeo ya mabadiliko ya tabia nchi

Utafiti wa wakulima wa kahawa uliofanywa miaka kadhaa iliyopita (Hanns R. Neumann Stifting 2010, Adp (2007)umeonyesha uelewa wao kwamba hali ya hewa inabadilika

pamoja na mwenendo wa mvua unaendelea kuwa sio wa kutabirika na hivyo kusababisha kushuka kwa tija.

Tafiti kadhaa za kisayansi zilizochapishwa kuhusu suala hili zinawasilisha mahitimisho yanayoelekea kupingana. Hata hivyo zinakubaliana katika vipengele vifuatavyo:

- Uzalishaji wa kahawa una uwezekano wa kuhamia kwenye miinuko ya juu zaidi kutokana na ongezeko la hali ya joto, ambayo ni sifa ya mabadiliko ya tabia nchi. Hili litaweza kusababisha mgawanyiko wa maeneo yanayozalisha kahawa nchini kote yenye kiwango cha chini cha mwinuko kwa uzalishaji wa Arabika, pengine kuongeza hadi mita 400 (Hagar, Schepp, University of Greenwidh 2011).

- Mabadiliko ya mwenendo wa mvua si dhahiri sana kutokana na tofauti muhimu kati ya modeli hizo. Kuna uwezekano kwamba mabadiliko ya tabia nchi yataongezeka sambamba na mzunguko wa EI Ninyo/la Nina. Hili litasababisha kungezeka kwa majanga ya hali ya hewa (ukame, mafuriko, n.k),. Mvua za kiholela zinaweza kuwaathiri sana wakulima wa Tanzania kwa vile ni 3% tu ya mashamba yana mifumo ya umwagiliaji.

Athari za aina hiyo za mabadiliko ya tabia nchi zingeweza kuwa na matokeo makubwa ya kiuchumi na kijamii kwa vile wakulima watatakiwa kurekebisha njia za utafutaji wao wa riziki; ambazo nazo zitakuwa na athari mbaya hasa katika mazingira ya miinuko kwa vile uzalishaji wa Kahawa utahitaji kupanuka kiuendelevu kwenda kwenye miinuko ya juu zaidi.

# 2. Mkakati wa Maendeleo ya Sekta ya Kahawa: Dira, Madhumuni na Misukumo ya Kimkakati

## 2.1 Dira ya Mkakati

Kutokana na mchakato shirikishi, wadau mbalimbali wa mnyororo wa thamani wa kahawa wamekubaliana mambo yafuatayo kuhusu mkakati:

> **“Tasnia ya Kahawa ya Tanzania inalenga kuwajengea wadau wote tasnia ya kahawa endelevu yenye kuleta faida na ya muda mrefu, inayozalisha kahawa ya Arabika na Robusta ya ubora wa hali ya juu inayokubalika kimataifa na kutoa mchango muhimu kwa uthabiti wa uchumi mkubwa, upunguzaji wa umaskini na uboreshaji wa riziki ya watanzania.”**

## 2.2 Dhumuni la Mkakati

“Dhumuni kuu la mkakati huu ni:

**“Kuongeza uzalishaji na ubora wa kahawa kitaifa ili kuboresha mapato katika mnyororo wote wa thamani, hususan wakulima wa kahawa”.**

Malengo ya kimsingi ni kama ifuatavyo:

- Ongezeko la uzalishaji wa kahawa safi kwa mwaka kutoka wastani wa sasa wa tani 50,000 hadi angalau tani 80,000 kufikia mwaka 2016 na tani 100,000 kufikia mwaka 2021.

- Kuongeza ubora wa kahawa utakaodhihirishwa na ongezeko la bei ya ziada kwenye masoko ya nje kutoka 35% ya jumla ya uzalishaji ya sasa hadi angalau 70% kufikia mwaka 2021.

- Hisa ya bei halisi (FOB) ya mkulima kwenye kahawa inayosafirishwa nje inaboreshwa kufikia angalau 75% ifikapo mwaka 2021.

## 2.3 Misukumo ya kimkakati

Ili kulifikia dhumuni hilo na kuchangia katika kufikia dira inayoshirikisha wadau wa kahawa kitaifa, misukumo ifuatayo imekubalika:

**Msukumo wa kimkakati wa 1: Kuongeza tija na uzalishaji wa kahawa wa jumla**

Kwa kuzingatia dhumuni la kuongeza uzalishaji hadi tani 80,000 kwa mwaka kufikia mwaka 2016 na tani 100,000 kwa mwaka kufikia mwaka 2021, kuna haja dhahiri ya kuboresha tija. Mavuno bora zaidi huongeza faida za kiuchumi katika kilimo cha kahawa kwa wakulima wadogo.

Hili litafanikiwa kwa kufanya shughuli kama za kufufua mashamba yaliyopo ya kahawa` (kupanda upya aina zilizoboreshwa), kuboresha kanuni za kilimo kupitia huduma za ugani zilizoboreshwa, kuongeza matumizi ya mbolea za viwandani pamoja na kudhibiti wadudu na magonjwa.

Hivi sasa uzalishaji wa kahawa nchini Tanzania unakadiriwa kuwa kwenye kg 150-200 za kahawa safi kwa hekta kwa Arabika au kama gramu 150 kwa mti mmoja. Uzalishaji kwa Robusta ni kama kg 550 kwa hekta. Matumizi ya njia mbalimbali zilizoorodheshwa hapo juu yana uwezo wa kuongeza uzalishaji angalau mara mbili kutoka wastani wa sasa wa kg 200-300 kwa hekta hadi kg 400-500 kwa hekta. Kuongeza tija kutahitaji jitihada kadhaa, zikiwemo: uelimishaji na matumizi ya kanuni bora za kilimo, matumizi ya pembejeo zinazofaa kama vile mbolea za viwandani, viuakuvu na viuatilifui, na muhimu zaidi ni kupanda tena aina bora zinazohimili magonjwa ili kubadilisha mibuni iliyozeeka.

Katika kiwango cha chini zaidi, upandaji wa mashamba mapya ya kahawa (hususan mashamba makubwa) ungeweza kuongeza uzalishaji wa kitaifa. Kuna mikoa kadhaa inayofaa kwa upanuzi wa kahawa nchini Tanzania, hii ni Mara, Kigoma, Rukwa, Iringa, Manyara, Tanga, Morogoro na Mwanza. Uchunguzi wa awali unaonyesha kwamba hekta 15,000 zipo kwa ajili ya upanuzi wa kahawa katika mikoa iliyotajwa hapo juu. Kuwavutia wakulima katika maeneo ya upanuzi waweze kuona faida za kulima kahawa ni changamoto kwa wadau wote hasa ukichukulia miaka miwili hadi mitatu (2-3) ya kipindi cha kuanzia hadi kuvuna kahawa.

<u>Viashirio vya mafanikio/ufanisi</u>

- Wastani wa mavuno ya zao la kahawa kwenye ngazi ya taifa utaongezeka kufikia angalau kg 450 za kahawa safi kwa hekta hadi kufikia mwaka 2021 (ongezeko la +100%).

- Angalau hekta 10,000 mpya za kahawa zitapandwa kufikia mwaka 2021

**Msukumo wa kimkakati wa 2: Kuboresha Ufanisi wa mnyororo wa thamani**

Wazalishaji wa kahawa wangeweza kupata hisa kubwa zaidi za bei za usafirishaji nje iwapo mfumo wa ndani wa masoko ungeboreshwa. Maeneo makuu ya kuangaliwa ili kuwahakikishia wakulima wanapata mapato bora zaidi yamependekezwa kama ifuatavyo:

a) Kushughulikia masuala kuhusiana na gharama za uendeshaji (usafiri, vikwazo vya kiutawala, usimamizi wa hatari za bei)
b) Kupunguza mwingiliano na urefu wa mnyororo wa thamani kunawezesha wakulima kuyafikia masoko bora zaidi
c) Kuhamasisha uwazi kupitia mfumo wa taarifa za masoko bora zaidi (watendaji, bei, wingi)
d) Kuboresha utawala wa mnyororo wa thamani kupitia mchakato wa wadau binafsi na umma.
e) Kuimarisha ufanisi wa ushirika/wanunuzi kwa kuwajengea uwezo
f) Kuwawezesha kwa mikopo na punguzo la hatari ya bei (kuongezeka kwa kasi ya usafirishaji wa kahawa kutoka shambani hadi nje ya nchi).

Mazingira ya biashara yaliyoboreshwa yangeweza kutoa fursaza kiuchumi za sekta ya kahawa ili kuruhusu uwekezaji mkubwa kwenye mnyororo wa thamani

SHERIA YA KAHAWA, kanuni na mikakati ya masoko inapaswa kufanyiwa marekebisho mara kwa mara kuhimiza ushiriki wa sekta na kuhakikisha ufungamano na mazingira ya biashara yanayobadilika. Ili kuhimiza uwekezaji zaidi katika kahawa hususan maeneo ya kodi, taratibu za forodha na umiliki wa ardhi, zinahitaji kupitiwa upya. Uboreshaji wa kazi muhimu za usaidizi na miundombinu pia ni muhimu, kwa mfano bandari, muda wa kusafiri hadi kwenye maeneo ya masoko makuu. Ufuatiliaji na usimamiaji wa kanuni unapaswa kuzingatia kujenga kiwango cha usawa wa kufanya kazi kwa ushindani wa kibiashara. Kuimarisha vyama vya ushirika na uwezekano wa matumizi ya mfumo wa Stakabadhi ya Mazao Ghalani (WHS) pia kungeweza kuboresha mazingira ya biashara.

**Viashirio vya mafanikio**

- Hadi kufikia mwaka 2021 wastani wa muda unaohitajika kusafirisha kahawa kutoka shambani hadi kufika bandarini unapunguzwa kutoka wastani wa meizi mitatu (3) hadi chini ya miezi miwili (2).
- Hadi kufikia mwaka 2021 hisa za wastani wa gharama za kufanya biashara kutoka shambani hadi bandarini umepunguzwa kutoka 35% za sasa hadi 25%

**Msukumo Mkakati wa 3: Kusaidia uboreshaji wa jumla wa ubora wa kahawa**

Bei za thamani ya nyongeza zinaweza kuongezwa kwa kuzalisha kahawa ya ubora zaidi. Hili litahitaji wakulima kukubali kanuni bora za kilimo/ uvunaji na baada ya uvunaji pamoja na kuboresha matumizi ya vifaa vya usindikaji, hususan CPU.

Mkakati huu unatambua fursa za kuboresha ubora wa jumla wa kahawa ya Tanzania, kupitia:

- Maendeleo ya wazi kuhusu kanuni za ubora kwa kushirikiana kati ya umma na sekta binafsi
- Upangaji bei unaozingatia ubora katika ngazi ya shamba
- Kuwajengea wakulima uwezo na kuwasaidia vifaa vya uzalishaji
- Kusaidia uanzishaji wa CPU pale inapofaa
- Ujumuishaji wa matumizi ya udhibiti binafsi wa ubora katika ushirika/wanunuzi kwa kutumia zana zinazofaa (kipima unyevu, mizani, n.k)

Pia, kwa kuzingatia maendeleo ya hivi karibuni kuelekea kwenye kusafirisha kahawa ya Robusta na uibukaji wa masoko maalumu (niche markets), uanzishaji wa Robusta iliyooshwa kikamilifu unaweza kufanyiwa majaribio.

**Viashirio vya ufanisi**

- Hadi kufikia mwaka 2021 angalau 70% ya kahawa inayozalishwa nchini Tanzania ni ya madaraja ya 1-7 (kwa mujibu wa uainishaji wa madaraja ya kahawa Tanzania).
- Hadi kufikia mwaka 2021 angalau 75% ya kahawa ya Arabika inayozalishwa Tanzania inasindikwa kupitia CPU.

**Msukumo wa Kimkakati wa 4: Kutafuta fursa mpya za masoko , ikijumuisha maendeleo ya Kahawa endelevu**

Kwa kuzingatia uwezo wa ubora wa kahawa ya Tanzania, kuna fursa kadhaa za kuchunguza ili kujenga thamani ya kushirikiana kwa wadau wote wa tasnia hii.

Wakati huohuo, kuna haja ya kuhakikisha tasnia ya kahawa endelevu ya muda mrefu kwa kushughulikia changamoto katika maeneo ya mazingira, ajira kwa watoto, usawa wa jinsia na ushiriki wa vijana katika kilimo cha kahawa. Kuwatia moyo wakulima kuongeza uzalishaji wa kahawa endelevu, sio tu kutakuwa na manufaa kwa sekta ya kahawa Tanzania kwa muda mrefu kwa kuhakikisha uhifadhi wa mazingira na usawa wa kijamii na kiuchumi na kijinsia, bali pia kutaweza kutoa fursa za kiuchumi na kutafuta bei za thamani ya juu kwenye masoko ya kimataifa.

Mwendelezo wa uhamasishaji wa kahawa ya Tanzania nje, ukijumuisha masoko mapya yanayoibukia (China, India, Brazili, Ulaya ya Mashariki, Pasific Asia, n.k) pia ungeleta faida nyingi za kiuchumi pamoja na maendeleo ya ubia wa kiuchumi na nchi zinazohusika (Japan, Marekani, Ulaya n.k.).

Hatimaye, ongezeko la thamani pia linaweza kufanikiwa kwa kuzalisha na kuuza kahawa kwa mfano kahawa iliyokaangwa, kahawa iliyokaangwa na kusagwa na kahawa ya unga kwenye masoko ya ndani/ya kanda. Jitihada nyingine zingeweza kusaidia maendeleo ya unywaji wa ndani.

<u>Viashirio vya mafanikio:</u>

- Hadi kufikia mwaka 2021 kiwango cha chini cha 50% ya kahawa inayozalishwa nchini Tanzania kitakuwa “endelevu” (k.m UTZ, 4C. FLO, Rain Forest Alliance, Oganiki).

- Hadi kufikia mwaka 2021 unywaji wa ndani utaongezeka nchini Tanzania na kufikia angalau tani 10,000 (za kahawa safi).

# 3. Mpango wa Utekelezaji wa mkakati

Katika kuandaa mkakati huu, wadau wamejaribu kuunganisha na mipango ya utekelezaji ya baadaye ili kuhakikisha kwamba mkakati hautabaki kuwa wa kinadharia. Mkakati huu unapaswa kuwa mwongozo halisi wa kuratibu uboreshaji wa tasnia ya kahawa. Shughuli kadhaa zilibainishwa chini ya kila msukumo unaozingatia uchanganuzi wa mapungufu (Nini kinafanyika hivi sasa? Ni uzoefu upi tunaoweza kuutumia kwa manufaa yetu?). Pia, wadau wamekubaliana kuhusu muda wa uwezekano wa utekelezaji, programu za vipaumbele vya kutekelezwa (upangaji vipaumbele wa shughuli) na wamebuni makadirio ya gharama za utekelezaji na matokeo/manufaa yanayowezekana ya kiuchumi na kijamii.

## 3.1 Shughuli kuu za utekelezaji

Shughuli muhimu za kufanikisha dhumuni hilo ni kama zilivyoelezwa hapa chini:

**Msukumo wa kimkakati wa 1: Kuongeza uzalishaji na tija**

Kiwango kikubwa cha uzalishaji kitatokana sanasana na kuboresha mavuno miongoni mwa mashamba ya kahawa yaliyopo. Kiwango hiki kikubwa cha uzalishaji kitafikiwa kwa kubadilisha mibuni iliyozeeka na kupanda miche bora inayostahimili magonjwa na inayozaa zaidi. Hili linaweza kufanyika tu kwa kushirikiana kwa karibu kati ya utafiti, huduma za ugani, na asasi za wazalishaji wa kahawa zilizopo. Uzoefu kutoka nchi nyingine unaonyesha kwamba nguvu zaidi zisielekezwe tu kwenye kuzalisha miche ya aina bora kwa wingi lakini pia kuendeleza huduma za ugani pamoja na kung'oa/upandaji upya wa kahawa na utumiaji wa kanuni bora za kilimo. Uanzishaji wa mtandao wa vitalu vya miche bora ya kahawa utakuwa ni mwanzo wa mafanikio pamoja na uwezo wa kuanzisha motisha za kiuchumi kwa wakulima ili kweli kufufua matumaini ya wakulima. Kwa kuzingatia kwamba mibuni mipya iliyopandwa itaanza kuzaa baada ya miaka minne, kuna haja ya kufidia upotevu wa mapato kwa kulipa fidia (pengine kwa kutoa fidia ya mbolea au viuatilifu) pamoja na mazao ya muda mfupi (maharage ambayo yanaweza kutoa kipato na wakati huohuo yakirutubisha udongo).

Uzalishaji pia, utaboreshwa kupitia upatikanaji mzuri zaidi wa pembejeo zenye ubora (mbolea, viuatilifu n.k). Hili litahitaji uchanganuzi wa udongo ambao utabainisha aina za pembejeo za kutumia, vifaa bora na upatikanaji wa mtaji kuwawezesha wakulima kutumia pembejeo. Uwezeshaji wa wakulima kupata pembejeo utahitaji kuratibiwa kupitia programu ya mbolea za kahawa; hii itakuwa ni fursa ya kuwashirikisha wagavi wa sekta binafsi.

Uwezeshaji wa matumizi ya kanuni bora za kilimo (kupogoa, uwekaji wa matandazo, kupalilia, matumizi sahihi ya miti ya kivuli, n.k) utakuwa umetilia maanani miongozo sahihi ya kiagronomia katika ngazi ya taifa/ngazi za mikoa na wilaya pamoja na kushirikisha maofisa ugani katika masuala maalumu ya agronomia ya kahawa.

Utekelezaji wa kanuni bora za kilimo, matumizi ya pembejeo na ufufuaji wa kahawa kwa kiwango cha juu vinategemewa kuongeza wastani wa mavuno kutoka kg 200-250 za kahawa safi kwa hekta hadi wastani wa angalau kg 350 kwa hekta ifikapo mwaka 2016 (+55%) na kg 450 kwa hekta ifikapo mwaka 2021 (+100%). Mchanganuo wa makisio kwa kila eneo la uzalishaji umeonyeshwa hapa chini.

| Msingi (2011) | | | | Madhumuni (2021) | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Chanzo: TCB 2011* | | | | | | | | |
| Eneo | Mavuno (kg/hekta) | Eneo (hekta) | Uzalishaji | Eneo | Mavuno (kg/hekta | Eneo (hekta) | Uzalishaji | Ongezeko |
| Kaskazini | 90 | 83000 | 7470 | Kaskazini | 270 | 83000 | 22410 | +200% |
| Kagera | 550 | 39000 | 21450 | Kagera | 850 | 39000 | 33150 | +55% |
| Mbeya | 220 | 51000 | 11220 | Mbeya | 450 | 53500 | 24075 | +105% |
| Ruvuma | 300 | 35000 | 10500 | Ruvuma | 600 | 37500 | 22500 | +100% |
| Nyingine | 150 | 21000 | 3150 | Nyingine | 250 | 26000 | 6500 | 67% |
| JUMLA | | 229000 | 53790 | JUMLA | | 239000 | 108635 | |
| **Wastani wa mavuno Kwa hekta** | | | **235** | | **Wastani wa mavuno** | **455** | | |

**Baadhi ya tarakimu zinaweza kuonekana kuwa chini hasa kutokana na ukadiriaji wa kupita kiasi wa maeneo ya kahawa (Je, mibuni michache kwenye hekta moja ichukuliwe kama hekta moja ya shamba la kahawa?).*

Idadi iliyokadiriwa ya miche milioni 20 itahitajika kwa mwaka kwa ajili ya upandaji upya kwa kiwango kikubwa pamoja na kuimarisha, ukizingatia kwamba uwezekano wa kuharibika kwa miche kwenye bustani na mashambani (Inakadiriwa kuwa kiwango cha uponaji wa miche ni 70% kama wastani iwapo kanuni bora za kilimo zimefuatwa). Kwa hivi sasa, maeneo ya upanuzi yatabainishwa katika wilaya mbalimbali kwa lengo la kuanzisha hekta 10,000 za mashamba mapya ya kahawa ifikapo mwaka 2021.

**Shughuli zitakazotekelezwa ili kufikia dhumuni hilo:**

| Namba | Maelezo ya Shughuli | Wakala Kiongozi | Hali |
|---|---|---|---|
| 1.1 | Kuanzisha programu ya Kitaifa ya kufufua kahawa kwa kiwango cha juu kwa kupanda aina bora mpya za kahawa na usambazaji wa mbolea kama mpango wa fidia | | |
| 1.1a | Kuongeza kasi ya uzalishaji na usambazaji wa miche ya aina bora ya kahawa ili ziwafikie wakulima wote wenye kuhitaji miche | TaCRI | Inahitaji Kuongezwa |
| 1.1 b | Kusaidia upandaji upya wa aina bora za kahawa mashambani (pamoja ulengetaji wa mibuni) na usambazaji wa mbolea kama fidia ya upotevu | Itabainishwa | Haipo |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1.2 | Kusaidia usambazaji wa kanuni bora za kilimo kwa wakulima wa kahawa nchini kote ili kuongeza uzalishaji/tija katika namna endelevu. | | |
| 1.2 a | Kuanzisha miongozo ya kitaifa ya kiagronomia ya kilimo cha cha kahawa kupitia mchakato wa wadau wengi kwa kuzingatia kanuni bora za kilimo zilizopo na mapendekezo kutoka taasisi za utafiti | TaCRI? | Tayari ipo Itaunganisha |
| 1.2 b | Kufanya tathmini ya matokeo ya mabadiliko ya tabia nchi kwenye maeneo ya uzalishaji wa kahawa na kushauri kuhusu hatua za kurekebisha/kupunguza na mapendekezo yanayo hitajika kwenye kanuni za kilimo bora zilizopo | TaCRI? | Baadhi ya takwimu Zipo/ kukusanywa |
| 1.2 c | Kuimarisha mahusiano kati ya Utafiti na huduma za ugani za wilaya ili kupanua wigo wa uenezaji wa agronomia ya kilimo cha kahawa nchini kote na ushauri wa kisasa uliofanywa | TaCRI? | Tayari vipo kuzidishwa |
| 1.2 d | Kuanzisha mtandao wa nchi nzima wa maofisa ugani wa kahawa (kwenye ushirika, waendeshaji binafsi, makundi ya wakulima, n.k) kupitia Mafunzo ya wakufunzi na kusaidia mafunzo ya mara kwa mara katika ngazi ya kijiji, ikiwa ni pamoja na mashamba ya mfano | Kubainishwa | Tayari upo Tumia AZISE Kuongezwa |
| 1.3 | Kuwezesha upatikanaji wa pembejeo na utunzaji wake wa kimantiki ili kupunguza gharama za uzalishaji wakati huo ukihifadhi mazingira | | |
| 1.3 a | Kufanya uchanganuzi wa udongo na majani ili kutoa mapendekezo kwa kila mkoa kuhusu matumizi ya mbolea inayofaa na matumizi ya pembejeo nyingine | Kubainishwa | Tayari ipo Kuongezwa |
| 1.3b | Kuanzisha mnyororo wa ugavi unaowiana na endelevu wa mbolea zilizothibitishwa, mashine, zana za kilimo, viuatilifu, sumu ya magugu na viuakuvu vilivyopendekezwa kwa kilimo cha kahawa kupitia programu iliyoratibiwa ya pembejeo | Kubainishwa | Haipo |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1.4 | Kuhamasisha uanzishaji wa mashamba mapya ya kahawa katika maeneo yenye uwezo mkubwa wa upanuzi, pengine mashamba yawe ya vijana wajasiria mali wa kilimo | Kubainishwa | Haipo |
| 1.4a | Kubainisha maeneo yanayofaa kwa uzalishaji wa kahawa ya ubora wa hali ya juu | Kubainishwa | Haipo |
| 1.4 b | Kufikiria uwezekano wa kuanzishwa kwa mfuko wa maendeleo ya kahawa | Kubainishwa | Haipo |
| 1.4 c | Kuangalia uwepo wa masoko kwenye maeneo mapya ya uzalishaji | Kuanzishwa | Havipo |
| 1.4.d | Kuanzisha na kusaidia mpango wa umwagiliaji maji | Kubainishwa | Haipo |
| 1.4. e | Kuvutia uwekezaji na kuanzisha kiasi cha hekta 10,000 za mashamba mapya ya kahawa | Kubainishwa | Haupo |
| 1.4 f | Kuboresha ushiriki wa vijana na kuongeza nafasi za kazi za kahawa | Kubainishwa | Haupo |

**Msukumo wa kimkakati wa 2:** Ub**oreshaji ufanisi wa mnyororo wa thamani**

Mazingira ya biashara na kanuni husika za kahawa vinahitaji kukuza tasnia endelevu ya kahawa iliyo imara na ya kiushindani. Majukumu yanayowahusu wadau katika mnyororo wa thamani yanahitaji kubainishwa ili kila mmoja aweze kuchangia kwa: kuongeza thamani, kupunguza gharama za biashara, na kuongeza kasi ya kusafirisha kahawa kutoka hatua moja ya mnyororo kwenda nyingine.

Kupunguza gharama za biashara pamoja na vikwazo mbalimbali vya kati kutaboresha ushindani katika sekta pamoja na mapato ya juu zaidi kwa wadau wote wa tasnia ya kahawa na hususan wakulima. Wakulima wanahitaji kupata mapato yanayolingana na hali halisi ya kahawa yao. Hii si njia tu ya kupunguza umaskini vijijini na kuboresha riziki, bali pia ni motisha muhimu kwao kuwekeza katika kuongeza tija na ubora.

**Shughuli za kutekelezwa ili kufanikisha dhumuni hilo:**

| **Namba** | **Maelezo ya shughuli** | **Wakala Kiongozi** | **Hali** |
|---|---|---|---|
| 2.1 | Uhamasishaji wa muundo wa jumla wa udhibiti unaovutia na unaowezesha kwa ajili ya wadau wa kahawa | | |
| 2.1a | Uhamasishaji uwekezaji wa sekta binafsi katika mnyororo wa thamani | TCB? | Upo Kuongezwa |
| 2.1b | Uboreshaji wa utawala wa sekta kwa kuanzisha kamati za wadau wengi kwenye ngazi za kitaifa na kikanda ili kutekeleza kazi za pamoja miongoni mwa wadau | TCB? | Upo Kuongezwa |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 2.1c | Uchunguzi wa fursa za kuangalia mazingira ya kodi yanayopendwa na yaliyo patanifu katika ngazi zote | TCB? | Zipo Kuongezwa |
| 2.1d | Kubuni mbinu nzuri za kupunguza gharama za usafirishaji, vifaa vya kufungashia na kodi za nishati | TCB? | Zipo Kuongezwa |
| 2.1e | Kuhakikisha uzingatiaji wa kanuni zilizorekebishwa ili kuboresha ushindani wa bei za mashambani | TCB? | Zipo Kuongezwa |
| 2.1f | Kusaidia uboreshaji wa sera/taratibu kuhusu muda na umiliki wa ardhi ambazo zitawanufaisha wakulima wa kahawa | TCB? | Zipo Kuongezwa |
| 2.2 | Kuboresha utendaji wa mfumo wa ndani wa soko, ikijumuisha mnada wa Moshi | | |
| 2.2a | Kuendesha ushauri wa binafsi/kitaifa kutathmini mageuzi yanayowezekana ili kurahisisha taratibu na kupunguza muda wa kusafirisha kahawa kutoka shambani hadi usafirishaji nje/bandarini | TCB? | Upo Kuendelezwa |
| 2.2b | Uboreshaji wa mnada ili kuvutia washiriki zaidi | TCB? | Upo kuongezwa |
| 2.2c | kuchunguza ushiriki wa mbali kwenye minada ya Moshi | TCB? | Haupo |
| 2.2d | kufikiria uingizaji katika mfumo wa upangaji madaraja uliopo/mifumo ya uainishaji wa kahawa | TCB? | Upo Kuongezwa |
| 2.3 | Kuhamasisha kilimo cha kahawa kama biashara na kuboresha uwezo na utawala bora wa vyama vya wakulia | | |
| 2.3a | Kuboresha upatikanaji wa mtaji na utaalamu wa jumla juu ya fedha na usimamizi hatarishI (vyama vya wakulima) | Kuainishwa | Upo Kuongozwa |
| 2.3b | Kufundisha wakulima kuhusu elimu ya msingi na uwekaji akiba ili kuongeza welewa wa gharama na mapato | Kuainishwa | Kupo Kuongezwa |
| 2.3c | Kusambaza taarifa dhahiri kuhusu gharama zinazozikabili asasi/vyama vya wakulima: Iweke alama teule ya ulinganishaji mifanano na ufafanuzi wa makundi /vyama vya ushirika vinavyotenda vibaya na vizuri kabisa | Kuainishwa | Zipo Kuongezwa |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 2.3d | kutoa taarifa kwa kulima kuhusu haki na wajibu wao kama wanachama wa asasi za wakulima na chini ya Sheria ya Kahawa | Kuainishwa | Ipo Kuongezwa |
| 2.3e | Kuwezesha wenye mikataba ya utoaji huduma tanzu/huduma za kahawa kupitia ubia wa umma na binafsi | Kuainishwa | Upo Kuongezwa |
| 2.4 | <u>Kuboresha mfumo wa uwazi kwa kusimamia utoaji wa taarifa</u> | | |
| 2.4a | Kufanya sensa ya mara kwa mara kuhusu uzalishaji, ekari, idadi ya mibuni, miundombinu iliyopo, ikijumuisha CPU | TCB? | Ipo Kuongezwa |
| 2.4b | Kusajili wakulima wa kahawa na kuwapa vitambulisho | TCB? | Upo kuongezwa |
| 2.4c | Kuwepo na kumbukumbu husishi za tasnia ya kahawa pamoja na mfumo halisi wa usambazaji taarifa | TCB? | Zipo ongezwa |
| 2.4d | Kuongeza mawasiliano ya taarifa ya bei za kahawa kwa wakulima kupitia magazeti, intaneti, simu za viganjani, redio na televisheni | TCB? | Yapo Kuongezwa |

**Msukumo mkakati wa 3**: **Kusaidia uboreshaji wa ubora wa kahawa**

Hivi sasa, kahawa ya Tanzania inapata bei ya thamani ya juu ya karibu 35% ya kahawa inayozalishwa. (Chanzo: TCB 2011)

Kahawa ya Tanzania inaweza kupata bei za juu zaidi kwenye soko, kwa kuboresha mbinu za usindikaji na uzingatiaji wa kanuni bora wakati wa kuvuna/baada ya kuvuna. Nchini Tanzania kiasi cha 11% ya kahawa husindikwa katika mitambo ya kati ya kumenyea kahawa wakati 89% husindikwa nyumbani (Hans R. Neumann Stiftung). Kwa kahawa inayosindikwa nyumbani, kutokana na kutozingatia kanuni bora, ubora wa kahawa unatofautiana hivyo kuwa kikwazo kikubwa kwa wanunuzi wakubwa wa kimataifa. Hivi sasa, sehemu kubwa ya kahawa ya Tanzania hutumika katika kuongeza ladha wa kahawa nyingine kwa sababu kiasi kinachozalishwa kitaifa ni kidogo pamoja na ubora kutofautiana. Kwa sababu hizo wakaangaji wakubwa wanashindwa kuiendeleza kahawa ya Tanzania kama kahawa yenye asili ya kipekee.

Uboreshaji wa ubora wa kahawa inayozalishwa kuzingatia matumizi ya kanuni bora za uvunaji/baada ya uvunaji pamoja na kuongeza kiasi cha kahawa iliyotayarishwa kupitia mitambo ya kati ndiyo kipaumbele.

**Shughuli za kutekelezwa ili kufanikisha dhumuni hilo:**

| Namba | Maelezo ya shughuli | Wakala kiongozi | Hali |
|---|---|---|---|
| 3.1 | Kuunga mkono uboreshaji kwa kujenga uwezo na zana zilizoimarishwa kwa ajili ya wazalishaji | | |
| 3.1a | Kuainisha miiko/viwango vya kitaifa kuhusu mchakato wa ubora kupitia ushauri wa binafsi na umma | Kuainishwa | Upo Kuongezwa |
| 3.1b | Kuanzisha utaratibu wa udhibiti binafsi wa ubora unaofanywa na vyama vya ushirika/wanunuzi wa kahawa na kusaidia zana zinazofaa (mita za unyevu, vipimo, n.k) | Kuainishwa | Upo Kuongezwa |
| 3.1c | Kuhamasisha upangaji bei unaozingatia ubora kwenye ngazi ya shamba | Kuainishwa | Upo Kuongezwa |
| 3.1d | Kutoa mafunzo ya kanuni bora za za utayarishaji na usindikaji wa kahawa | Kuainishwa | Yapo Kuongezwa |
| 3.1e | Kutoa mafunzo kwa waonjajji wa kahawa Katika mnyororo wa thamani | Kuainishwa | Yapo Kuongezwa |
| 3.1f | Kuongeza upatikanaji wa nyenzo za kuonjea kahawa katika ngazi ya mkoa ili kuboresha ubora | Kuainishwa | Vipo Kuongezwa |
| 3.1g | Kuandaa na kusambaza vifaa vya uelimishaji (vipeperushi, mabango, redio n.k) | Kuainishwa | Vipo Kuongezwa |
| 3.1h | Kusaidia zana za wakulima wanaotumia mashine za mikono za kumenyea /kukaushia kahawa hasa kwenye maeneo ambako CPUs haziwezi kuwekwa | Kuanishwa | Zilizopo Kuongezwa |
| 3.2 | Kukuza maendeleo ya CPU, kwa kahawa iliyooshwa kikamilifu, pale inapowezekana | | |
| 3.2a | Kusambaza taarifa kupitia tasnia hii juu ya manufaa ya kahawa iliyooshwa kikamilifu | Kuainishwa | Zipo Kuongezwa |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 3.2b | Kuanzisha mapendekezo ya sera ya kiufundi kupendekeza mahali panapofaa kwa ajili ya kusimika CPU pamoja na uchaguzi wa kutosha wa zana na mifumo ya ujenzi | Kuainishwa | Zilizopo kuongezwa |
| 3.2c | Kutumia fursa kwa ajili ya CPU ndogo zisizo na madhara kwenye mazingira na kusaidia usambazaji endelevu wa maji pamoja na urejeshaji fanisi wa maji machafu/uchafu wa kwenye mitambo | Kuainishwa | Zilizopo kuongezwa |
| 3.2d | Kutoa mafunzo kuhusu jinsi ya kuanzisha na kuendesha CPU (fedha, upangaji bei wa kahawa mbivu, n.k) | Kuainishwa | Yapo Kuongezwa |
| 3.2e | Kusaidia ujenzi wa CPU kupitia misaada pamoja na kushawishi kwa ajili ya dhamana ya mkopo kwa ajili ya uwekezaji wa mitaji katika CPU | Kuainishwa | Zipo kuongezwa |
| 3.3 | <u>Pale inapowezekana kusaidia maendeleo ya kijiji/kutoa mashine zinazo hamishika za kutoa maganda kwa ajili ya Robusta.</u> | | |
| 3.3a | Kuanzisha sera inayotawala ya mashine zinazo hamishika za kutolea maganda | Kubainishwa | Haipo |
| 3.3b | Kusambaza taarifa kwenye mnyororo mzima wa thamani kuhusu faida za kutumia mashine za ukoboaji katika ngazi ya kijiji | Kuainishwa | Haipo |
| 3.3c | Kutoa mafunzo kwa wakulima wadogowadogo ili kuanzisha na kuendesha, kwa namna inayofaa mashine zinazohamishika za ukoboaji wa Robusta | Kuainishwa | Haipo |
| 3.3d | Kushawishi kuhusu mikopo ya dhamana kwa ajili ya uwekezaji wa matumizi ya mitaji ya mashine zinazohamishika za ukoboaji | Kuainishwa | Hazipo |
| 3.3d | Kushawishi kwa ajili ya mikopo ya dhamana kwa ajili ya uwekezaji wa matumizi ya mitaji katika mashine zinazohamishika za kukobolea | Kuanishwa | Hazipo |

**Msukumo Mkakati wa 4: Kusaidia Wauzaji wa Kahawa ya Tanzania nje na kutafuta fursa mpya za masoko, ikiwa ni pamoja na kahawa endelevu**

Kuna umuhimu wa kuboresha uuzaji wa kahawa ya Tanzania nje kwenye masoko ya asili kupitia ubia wa pamoja na masoko mapya. Matakwa ya tasnia ya kimataifa inayohitaji kahawa endelevu inapaswa pia kuzingatiwa kwa vile wadau wakubwa wa kahawa duniani wanazidi kukazania kuongeza hisa ya kahawa endelevu wanayonunua. Ni muhimu kwa Tanzania kwenda sambamba na mabadiliko haya pamoja na kuhakikisha uhifadhi wa

mazingira na usawa wa kiuchumi/kijinsia katika siku za baadaye. Mwisho, masoko ya kanda pamoja na masoko ya nje siku za baadaye yangeweza kuwakilisha vyanzo muhimu vya mapato kwa tasnia ya kahawa Tanzania.

**<u>Shughuli za kutekelezwa ili kufanikisha dhumuni hilo:</u>**

| Na. ya shughuli | Maelezo ya Shughuli | Wakala Kiongozi | Hali |
|---|---|---|---|
| 4.1 | <u>Kuendeleza aina ya kahawa ya Tanzania na kuuza kahawa asilia ya Tanzania kwenye masoko ya nje</u> | | |
| 4.1.a | Kubainisha mkakati wa muda mrefu wa masoko | TCB? | Zipo Kuongezwa |
| 4.1b | Kutangaza kahawa ya Tanzania nje ya nchi kwa kushiriki kwenye maonyesho ya biashara na kampeni zinazolenga uhamasishaji | TCB? | Zipo Kuongezwa |
| 4.1.c | Kuendesha tafiti za masoko kuhusu masoko yanayoibukia na kusaidia maendeleo ya ubia wa kiuchumi | TCB? | Zipo Kuongezwa |
| 4.1.d | Kuendesha mashindano mengi ya kahawa na kutangaza matokeo yake Kimataifa | TCB? | Tayari yapo Kuongezwa |
| 4.2 | <u>Kuhamasisha uzingatiaji wa viwango vya mazingira na kijamii na kuongeza uzalishaji wa kahawa endelevu</u> | | |
| 4.2a | Kuendesha majadiliano ya wadau wengi kuhusu faida zilizopo za viwango vya mazingira na jamii | Kubainishwa | Havipo |
| 4.2b | Kuunga mkono uzalishaji wa kahawa endelevu (yaani UTZ, 4C,FLO, Rainforest, Oganiki, n.k) hasa kupitia huduma za ushauri | Kubainishwa | Hazipo |
| 4.2c | Kuwafundisha wataalamu wa ndani ili kupunguza gharama za ukaguzi/uthibitishaji wa bidhaa ya kahawa | Kubainishwa | Haipo |
| 4.2d | Kuhamasisha kanuni bora kabisa za mazingira, ikiwa ni pamoja na udhibiti husishi wa wadudu, mbolea za kioganiki/Asilia, n.k. | Kuainishwa | Zipo Kuongezwa |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 4.2e | Uboreshaji wa usawa wa kijinsia na ushiriki wa wanawake kwenye ngazi zote za mnyororo wa thamani | Kuainishwa | Tayari upo (Tumia AZISE kwa faida) Kuongezwa |
| 4.2f | Kuhakikisha kwamba hakuna ajira kwa watoto katika tasnia ya kahawa kitaifa | Kuainishwa | Tayari upo Kuongezwa |
| 4.3 | <u>Kuhamasisha matumizi ya ndani na uzalishaji wa kahawa ya kukaanga na kusaga inapokuwa na faida kiuchumi</u> | | |
| 4.3a | Kuhamasisha matumizi ya kahawa zilizokaangwa, kahawa iliyosagwa na kahawa ya matumizi ya haraka | Kubainishwa | Haipo |
| 4.b | Kuimarisha uwezo wa ndani wa tasnia ya ukaangaji na ufungashaji wa kahawa | Kubainishwa | Haipo |
| 4.3c | Kuhakikisha upatikanaji wa ndani wa kahawa yenye ubora | Kubainishwa | Haipo |
| 4.3d | Kuanzisha siku ya Taifa ya Kahawa Tanzania | Kubainishwa | Haipo |

## 3.2 Mfumo wa utekelezaji unaopendekezwa

Ili kufIkia Malengo Mkakati kama ilivyoelezwa katika mkakati, lazima kuwepo na ushirikiano wa karibu miongoni mwa wadau wote katika sekta ya kahawa kwa utekelezaji wa programu (mchakato wa wadau wengi). Mpango huu unatoa muhtasari wa maelezo ya jumla wa baadhi ya taasisi kuu za sekta ya kahawa na majukumu yake yanayotarajiwa katika utekelezaji.

### 3.2.1 Majukumu ya Taasisi za Wadau wa Kahawa

a) <u>Asasi za wazalishaji na wakulima wa kahawa</u>
Wakulima na asasi zao ndio kiini cha mkakati huu wa maendeleo ya kahawa. Wakulima wenyewe watahitaji kujihusisha na kuhusishwa chini ya uongozi mzuri ili kupanda tena aina bora za miche , wakitumia kanuni bora za kilimo na hatimaye, kuongeza uzalishaji. Watafanya hivyo iwapo tu watakuwa na imani kwamba watapata hisa halali ya mapato kwa kahawa yao (ufanisi ulioboreshwa wa mnyororo wa thamani) na kwamba uwekezaji wowote ule katika uzalishaji/ubora ulioboreshwa utaleta mapato mazuri zaidi.

b) <u>Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika</u>

Ina dhamana ya sera na mpango wa kilimo. Wizara inaweza kuhakikisha kwamba malengo ya mkakati wa tasnia ya kahawa yanaoanishwa na sera ya Kilimo ya Taifa, yanawasilishwa na kujadiliwa katika ngazi ya taifa na ndani ya Wizara na kuhakikisha kuna uhusiano na taasisi

nyingine kuu za serikali na sekta nyingine za mazao. Wizara pia itakuwa na nafasi kubwa kwa kuunga mkono mazingira mazuri kwa kilimo cha kahawa (kodi, kanuni, sera ya kilimo) na pengine kwa kusaidia utekelezaji wa mkakati kupitia njia mbalimbali (msaada wa kifedha, ruzuku kwa pembejeo za kahawa, utetezi kwa wafadhili wa kimataifa).

c) <u>Bodi ya Kahawa Tanzania (TCB)</u>

Jukumu la TCB ni muhimu sana kwa utekelezaji kwa vile inatarajiwa kuongoza uratibu wa jumla wa utekelezaji wa mkakati na katika kuhakikisha mawasiliano sahihi kati ya wadau wote wa tasnia hii (mchakato wa wadau wengi). Kwa kufanya hivyo, itahakikisha kwamba kazi shirikishi zinatekelezwa kama ilivyokusudiwa katika Sheria ya Kahawa na kanuni mpya za kahawa. Pia, itatoa masharti stahiki ya biashara yanayofaa kwa wadau wote na itajitahidi kuboresha utendaji katika mnyororo wa thamani (masoko ya ndani na kanuni za sekta). Hatimaye, jukumu la TCB litakuwa kutoa huduma za kiushauri na kukuza/kutangaza kahawa ya Tanzania kwenye masoko yaliyopo/masoko mapya.

d) <u>Taasisi ya Utafiti wa Kahawa Tanzania (TaCRI)</u>

TaCRI itatekeleza jukumu la msingi katika kutoa teknolojia stahiki kupitia utafiti na kuhakikisha usambazaji wake kwa wadau wote hususan, wakulima. Msisitizo utakuwa kwenye programu kubwa ya upandaji upya wa kahawa kwa kufanya kazi kwa pamoja na wadau binafsi na wa umma wa kahawa ili kuhakikisha madhumuni haya ya shauku yanakidhiwa kupitia uzalishaji na usambazaji fanisi wa miche ya aina bora. Pia, inatarajiwa kuratibu pamoja na wadau wengine watakao husika ili kuhakikisha upandaji upya wa miche bora inayotosheleza mashambani.

e) <u>Sekta binafsi- wafanyabiashara/wasafirishaji nje/wakoboaji/wakaangaji</u>

Kampuni za sekta binafsi (wanunuzi, wasindikaji, wasafirishaji nje, n.k) zinaweza kuwa nguvu kubwa ya msukumo katika utekelezaji halisi wa mkakati huu. Kupitia utekelezaji wa kazi za pamoja na ubia wa umma na binafsi, pande hizi zinaweza kushiriki katika kuboresha ufanisi wa mnyororo wa thamani na kuwa chombo muhimu cha kuwasilisha kanuni za kuboresha kilimo/uvunaji/kanuni za utayarishaji baada ya uvunaji shambani.

g) <u>Mamlaka za serikali za Mitaa (LGA)</u>

Mamlaka za serikali katika kila mkoa unaozalisha kahawa zitakuwa na jukumu la kuelekeza rasilimali na kugharamia kahawa kupitia mipango ya maendeleo ya kilimo na bajeti angalau 20% ya ushuru wa kahawa. Pia, wanaweza kushiriki katika uanzishaji wa mazingira yanayofaa kwa biashara kupitia upatanifu wa kodi na kanuni. Kwa nyongeza, serikali za mitaa zinaweza kusaidia katika kujenga mazingira yanayo hitajika kwa kuwekeza katika miundombinu kama barabara zinazoingia katika barabara kuu, upatikanaji wa maji na nyenzo za afya, ambazo zitahamasisha mazingira ya mkulima wa kiwango cha juu kabisa. Mamlaka ya Serikali za Mitaa pia zinawajibika, kuwaajiri na kuwapangia vituo mabwana shamba ili kuwashauri wakulima wa kahawa kuhusu kanuni bora za kilimo cha kahawa. Mwisho, Mamlaka ya Serikali za Mitaa zihamasishe na kufundisha juu ya uundwaji wa vyama vya ushirika vya uzalishaji wa kahawa miongoni mwa wakulima wa kahawa.


h) <u>Asasi Zisizo za Serikali (AZISE)</u>

AZISE kadhaa zina fursa pana ya utaalamu, fedha na rasilimali zilizotengwa kusaidia utekelezaji wa kazi zinazo changia moja kwa moja kwenye mkakati wa sekta ya kahawa. Asasi hizo zinaweza kutoa utaalamu zinapohitajika na kusaidia utekelezaji katika nyanja mbalimbali za mkakati. Kipengele kimoja kinachovutia ni kutumia mafanikio ambayo tayari

yamekwishapatikana katika baadhi ya miradi nchini kote kuboresha mbinu na kuhakikisha mafanikio makubwa zaidi.

### 3.2.2 Muundo wa wadau wengi kwa ajili utekelezaji wa Mkakati

Thamani ya mkakati ina jidhihirisha zaidi katika mchakato wa utekeelzaji – kuboresha kiwango cha ushirikiano na mazungumzo kati ya sekta binafsi na umma ili kuendeleza uwezo endelevu wa kushughulikia matatizo ya sekta – kama katika matokeo. Wadau wote walioorodheshwa awali (3.2.1) watahitaji kuratibu kupitia mikutano ya wadau wengi ya kanda/kitaifa ili kufanikisha lengo la mkakati. Mfumo wa uratibu ufuatao unapendekezwa.



## 3.3 Upangaji wa vipaumbele na makisio ya awali ya gharama

Mambo yafuatayo ya utekelezaji yalibainishwa na wadau na kupangwa kufuatana na umuhimu ili kutofautisha kati ya programu za vipaumbele ambazo zinapaswa kutekelezwa mapema iwezekanavyo na mambo mengine muhimu ambayo si ya lazima sana kufikia madhumuni. Uchanganuzi wa kina wa gharama na muundo wa programu vitaendelezwa zaidi na wadau katika hatua ya baadaye, makisio ya gharama za awali yametolewa kama rejea.

Programu tano zifuatazo zimebainishwa na wadau kama vipaumbele vya juu kabisa katika utekelezaji.

### 3.3.1 Programu ya 1 ya Kipaumbele: Kiasi kikubwa cha ufufuaji wa mashamba ya kahawa kwa kupanda aina bora za kahawa zenye mavuno mengi na zenye kuhimili magonjwa

Wadau wakuu wa utekelezaji:

- TaCRI
- TCB
- LGA
- AZISE
- Sekta Binafsi

| Shughuli | Kiashirio cha lengo | Gharama iliyokadiriwa (kwa Mwaka) |
|---|---|---|
| A1: Kuharakisha programu ya uzalishaji wa miche ya aina bora ya kahawa | Jumla ya miche bora milioni 20 itazalishwa kwa mwaka | Dola za Marekani milioni 8 |
| A2: Kusaidia ukarabati upya wa mashamba ya kahawa kupitia uoteshaji upya kwa kuondoa mikahawa isiyo na tija | Mikahawa milioni 10 ya aina bora inapandwa tena kwa mwaka | Dola za Marekani milioni 7 |
| **JUMLA (1)** | | **Dola za Marekani milioni 15** |

### 3.3.2 Programu ya 2 ya kipaumbele: Programu ya Kitaifa ya usambazaji wa kanuni bora za kilimo kwa wakulima wa kahawa ili kuhakikisha uzalishaji endelevu wa kahawa

Wadau wakuu wa utekelezaji:

- TaCRI
- TCB
- LGA
- AZISE
- Sekta Binafsi

| **Shughuli** | **Kiashirio cha Lengo** | **Gharama iliyokadiriwa (kwa mwaka)** |
|---|---|---|
| A1: Kuanzisha miongozo ya kitaifa ya kiagronomia ya kilimo cha kahawa kwa kuzingatia kanuni bora na mapendekezo kutoka taasisi za utafiti (ikijumuisha viwango endelevu) | Upatikanaji wa miongozo dhahiri ya kiagronomia ya kilimo kwa kila eneo la kilimo-ekolojia | Dola za Marekani milioni 0.2. |
| **A2:** Kuongeza programu ya kuelimisha wakulima kupitia maendeleo ya programu ya kitaifa ya Mafunzo kwa Wakufunzi kuhusu agronomia ya kilimo cha kahawa (vikiwemo viwango endelevu) | Angalau wakulima wa kahawa 45,000 watafundishwa kila mwaka kuhusu kanuni bora za kilimo, kupitia mafunzo vijijini | Dola za Marekani Milioni 6. |
| **JUMLA (2)** | | Dola za Marekani Milioni 6.2 |

### 3.3.3 Programu ya 3 ya Kipaumbele: Utumiaji wa hali ya juu wa ufanisi wa mnyororo wa thamani kupitia mchakato wa soko la ndani ulioimarishwa na mazingira ya biashara yaliyoboreshwa.

Wadau wakuu wa utekelezaji:

- TCB
- Sekta Binafsi
- LGAs
- Serikali

| **Shughuli** | **Kiashirio Lengo** | **Gharama iliyokadiriwa (kwa mwaka)** |
|---|---|---|
| A1: Kuendesha ushauri binafsi wa kitaifa na wa umma kutathmini mfumo wa kanuni zilizopo za udhibiti na kubainisha njia zinazowezekana za kuboresha ufanisi wa mnyororo wa thamani | Upatikanaji wa taarifa yenye mapendekezo bayana kutokana na ushauriano wa wadau wengi | Dola za Marekani milioni 0.2 |
| A2: Kutengeneza takwimu za tasnia na mfumo wa taarifa ya bei | Mfumo wa taarifa ukiunganishwa ambao unaruhusu kukusanya na kusambaza taarifa muhimu kuhusu uzalishaji, masoko na bei, unafanya kazi. | Dola za Marekani milioni 0.3 |
| A3: Kuongeza uwezo wa asasi za wazalishaji na kuboresha utawala wao | Asasi za wazalishaji 150 zifundishwe kila mwaka kuhusu kanuni bora katika nyanja za usimamizi, fedha na utawala | Dola za Marekani milioni 0.25 |
| A4: Kufundisha wakufunzi watakao fundisha wakulima kuhusu elimu ya msingi ya fedha na masoko ya ndani | Wakulima 6,000 wafundishwe kila mwaka kuhusu elimu ya msingi ya fedha na masoko ya ndani | Dola za Marekani Milioni 0.4 |
| A5: Kuwezesha mikutano ya wadau ya mara kwa mara kwenye ngazi za kitaifa na za ndani ili kuwawezesha wanachama wote wa mnyororo wa thamani na kuhakikisha ushiriki wao katika utawala wa sekta hii | Mikutano kwenye ngazi ya kitaifa na kila eneo la uzalishaji kufanyika kila baada ya miezi mitatu na kuruhusu wadau binafsi/umma wa mnyororo wa thamani kuyashughulikia masuala yaliyomo | Dola za Marekani milioni 0.2 |
| **JUMLA (3)** | | Dola za Marekani Milioni 1.35 |

### 3.3.4 Programu ya 4 ya Vipaumbele: Uboreshaji wa Ubora wa Kahawa kuzingatia kanuni bora za uvunaji, uandaaji na usindikaji wa kiwango cha juu

Wadau wakuu wa utekelezaji:

- TCB
- Sekta Binafsi
- AZISE
- LGAs

| Shughuli | Kiashirio cha Lengo | Gharama kadiri au (kwa mwaka) |
|---|---|---|
| A1: Kusaidia uimarishaji wa ubora kwa kuwajengea uwezo wazalishaji na kwenye mnyororo wote wa thamani | Wadau wakuu wa mnyororo wa thamani (ikiwa ni pamoja na TCB) pamoja na vyama 150 vya wazalishaji wafundishwe kila mwaka kuhusu masuala ya kanuni za ubora za utayarishaji, na baada ya mavuno | Dola za Marekani milioni 0.6 |
| A2: Kuongeza uzalishaji wa kitaifa wa kahawa ilyomenywa kwa kuweka CPU pale ambapo inawezekana kiuchumi | Baada ya ainisho la miongozo ya taifa CPU 30 zijengwe/ kukarabatiwa kila mwaka na wasimamizi wafundishwe ipasavyo | Dola za Marekani milioni 0.6 |
| A3: Kuzidisha ubora wa Robusta kwa kutoa zana zinazotosha na kusaidia ukoboaji unaohamishika | Mafunzo mahususi ya Robusta na msaada wa vifaa | Dola za Marekani milioni 0.4 |
| **JUMLA** | | Dola za Marekani milioni 2.5 |

### 3.3.5 Programu ya 5 ya Vipaumbele: Uhamasishaji wa Kahawa ya Tanzania kwa kuweka Chapa na Uendelevu

Wabia wakuu wa utekelezaji:

- TCB
- Sekta Binafsi
- AZISE
- LGAs

| **Shughuli** | **Kiashirio cha Lengo** | **Gharama iliyokadiriwa (kwa mwaka)** |
|---|---|---|
| A1: Kuendeleza Chapa ya Tanzania na kuhamasisha kahawa asili ya Tanzania kwenye masoko ya nje | Kushiriki katika maonyesho ya biashara na kuwepo na masomo ya masoko | Dola za Marekani Milioni 0.3 |
| A2: Kuhamasisha uzingatiaji wa viwango vya mazingira na uwajibikaji wa kijamii | Kuainisha mkakati wa uzalishaji wa kahawa endelevu na ubia na jitihada zilizopo | Dola za Marekani milioni 0.2 |
| A3: Kuza matumizi ya ndani na uzalishaji wa kahawa iliyokaangwa na kusagwa (pale inapowezekana) | Mpangilio wa matukio ya ukuzaji/mafunzo ya barista/mashindano ya uvunaji | Dola za Marekani milioni 0.2 |
| **JUMLA (5)** | | Dola za Marekani milioni 0.7 |

| Jumla ya gharama za programu ya kipaumbele (1) + (2) + (3) + (4) + (5) | Kadirio la gharama/ mwaka (Dola za (Marekani) |
|---|---|
| • **Gharama zilizokadiriwa** | **26,000,000** |

## 3.4 Mpangilio  wa mabadiliko yanayowezekana na matokeo ya mkakati Kijamii na Kiuchumi

Mipangilio ifuatayo inaonyesha kwamba kama mkakati huu wa kahawa ukitekelezwa, **unatarajiwa kuleta mapato ya ziada ya angalau  Dola za Marekani Milioni 150 kwa mwaka** kwa makadirio ya miaka 10 mfululizo (+ Dola za Marekani Milioni 223 kwa bei za sasa) kwenye tasnia ya kitaifa kutokana na mapato ya kusafirisha kahawa nje.  Kati ya jumla ya Dola za Marekani milioni 250  zinazozalishwa kwa mwaka na tasnia ya kahawa (Dola za Marekani Milioni 335 kwa  bei za sasa), angalau 75% zingesambazwa tena kwa wakulima wa kahawa.  **Hii  ingeongeza mapato ya kahawa karibia mara mbili** (**ongezeko la 95% ) ya kadirio la kaya 400,000,** hivyo kuchangia upunguzaji wa umaskini na kuijengea uwezo endelevu tasnia ya kahawa kujiendeleza.

### 3.4.1 Mpangilio wa mabadiliko  usiofaa

KAMA

Wadau wa kahawa hawaimarishi ushirikiano, hawatumii mkakati mmoja wa kuratibu juhudi na kuendeleza ufanyaji kazi pamoja , kugharamia utekelezaji wa mkakati wa pamoja hakutoshelezi.

HALAFU,

Miradi ya pekee (AZISE, TaCRI, TCB, n.k) imefanikiwa  kutoa matokeo na kuboresha utendaji wa maeneo mahususi kwenye mnyonyoro wa thamani (uzalishaji wa miche, uimarishaji wa ubora kwa vyama vichache vya ushirika n.k) lakini imeshindwa kupata matokeo endelevu ya kuleta “mabadiliko katika sekta”.

Uzalishaji nchini Tanzania umeendelea kupungua, hususan Kaskazini mwa nchi, kutokana na kuzeeka kwa mibuni na  kanuni za kilimo zisizo endelevu. Kukosekana kwa uratibu wa miradi/utafiti/huduma za ugani hausaidii kubadilisha kushuka kwa uzalishaji, kahawa inazidi kuonekana na wakulima kama shughuli ya kiuchumi ambayo, hakika hairuhusu kusaidia kujipatia riziki.  Wakulima wa kahawa wanaimarisha kanuni za  kilimo mseto , hivyo kuchangia kushuka kwa kasi kwa uzalishaji wa kahawa au wanang’oa mibuni (kwa sababu ya ardhi kuwa finyu). Katika maeneo ambayo hakuna mazao mengine yanayoweza  kuchukua nafasi yake (Kusini na Kaskazini  Magharibi mwa Tanzania), uzalishaji unaweza kuendelea kuendelezwa na kuwa wa faida pale ambapo mashamba  makubwa/mashamba chanzo yanaruhusu uwekezaji wa sekta binafsi na njia fanisi za masoko: Uzalishaji unaelekea kwenye bidhaa mbili zinazokinzana:

- Uzalishaji mdogo/bei ya juu kwa kahawa yenye ubora  wa  hali ya juu

- Kahawa “nyenzo” ainasafu kwa wingi wa uzalishaji inayonunuliwa tu kama mbadala rahisi kutoka kahawa laini ya Amerika ya kati ambayo faida yake kubwa ni bei ya chini na muda muafaka inapoingia sokoni

Kuwepo kwa muda mrefu kwa sekta ya kahawa Tanzania kuna hatarishwa na uzalishaji wa jumla kuwa mdogo sana kiasi kwamba wakaangaji hawaichukulii tena kama kiambata chenye uwezo katika aina yao ya kahawa.

### 3.4.2 Mpangilio mzuri wa mabadiliko

KAMA

Wadau wa kahawa wanatumia mkakati unaofanana katika kuratibu juhudi zao na kuendeleza kufanya kazi kwa pamoja na kugharamia utekelezaji halisi wa mkakati wa pamoja unaokidhi

HALAFU

Ongezeko la uzalishaji pamoja na ubora vimezalisha mapato ya ziada yafuatayo kwenye mnyororo wa thamani:

Mapato kutokana na ongezeko la uzalishaji (+ tani 50,000)

X

Kuboreshwa kwa thamani ya usafirishaji nje katika kipindi cha miaka 10 ya makadirio
(Dola za Marekani 2.5 kwa kg)[1].
= Dola za Marekani, milioni 125 kwa mwaka

+

+ Uboreshaji wa bei za kahawa kwa uzalishaji wa kahawa wa sasa (tani 50,000)
= Dola za Marekani milioni 25 kwa mwaka

Sambamba na hilo, gharama za uzalishaji zimepungua kwa kiasi kikubwa nchini kote kutokana na usambazaji wa aina bora (pembejeo chache zaidi, upotevu mdogo wa uzalishaji) ambao huwaongezea faida wakulima wa kahawa. Utekelezaji wa mkakati huu na ushirikiano mzuri kati ya umma na sekta binafsi huboresha ufanisi wa mifumo ya masoko ya ndani inayosababisha kupungua kwa gharama za biashara, hivyo kuwa na mapato mazuri zaidi kwenye mnyororo wa thamani ikiwa ni pamoja na wakulima. Faida ya kiuchumi iliyoboreshwa ya uzalishaji wa kahawa hujenga motisha kwa ajili ya uwekezaji zaidi unaosababisha kujigharimia katika uboreshaji endelevu wa utendaji wa sekta ya kahawa. Hali ya kiuchumi na kijamii ya idadi ya watu wa vijijini nchini Tanzania inaboreshwa kwa kiasi kikubwa kutokana na kuboreshwa kwa masoko ambayo huruhusu kiasi cha 75% ya faida ya bei ya FOB inayorudi kwa wakulima wa kahawa, inayosababisha usambazaji tena wa jumla ya mapato ya kiasi cha Dola za Marekani Milioni 187,5 kusambazwa miongoni mwa wakulima 400,000 wanaowakilisha ongezeko la + 95% la kadirio la mapato yao ya sasa ya kahawa. Ziada hii ya pato taslimu (+Dola za Marekani 227 kwa kila mkulima) huchangia kwenye punguzo endelevu la umaskini na upatikanaji wa huduma za msingi, kama vile elimu, afya, maji/ usafi wa mazingira.

Uwezo chanya hujengwa wakati mapato ya kodi pia yanapozalishwa kwa ajili ya kusaidia programu za sekta (TCB, TaCRI, nyingine) ambazo kwa upande wake huruhusu uwekezaji zaidi katika tasnia. Mamlaka za Serikali za Mitaa pia hunufaika kutokana na mapato yaliyoboreshwa yanayowaongezea uwezo wa kusaidia uzalishaji wa kahawa kupitia huduma za ugani.

Kuongezeka kwa uzalishaji na ubora, pamoja na kuboreshwa kwa mazingira ya biashara huvutia tasnia ya kimataifa ya kahawa, kuongeza uwekezaji na kuendeleza zaidi sekta ya kahawa ya Tanzania.

[1] Makadirio ya kihafidhina ya 30% za Robusta iliyouzwa kwa Dola za Kimarekani 1,6/kg na 70% ya Arabika iliyouzwa kwa senti za Kimarekani kwa ratili (lb) kwa kuzingatia wastani wa bei katika miongo mitatu iliyopita pamoja na dofrenshia.

## Viambatanisho

### Kiambatanisho cha 1: Mchanganuo wa "SWOT" wa Sekta ya Kahawa Tanzania

Ili kuzishughulikia changamoto katika sekta, uchanganuzi wa SWOT umefanyika kwa pamoja na wadau wakuu katika tasnia. Jedwali hili linatoa muhtsari wa matokeo makuu ya majadiliano.

| **Uwezo/Nguvu** | **Udhaifu** | **Fursa** | **Vikwazo/Vitishio** |
|---|---|---|---|
| Ardhi tele inayofaa kwa kilimo cha kahawa | Uzalishaji mdogo | Tanzania iko katika kundi la kahawa laini ya Kolombia | Mabadiliko ya tabia nchi/hali ya hewa isiyotabirika |
| Hali nzuri kwa ajili ya uzalishaji | Huduma duni za ugani na ushauri usiotosheleza | Uwezo wa kupata bei za thamani ya juu | Kuongezeka kwa gharama za pembejeo |
| Ubora wa hali ya juu wa kahawa | Mifumo isiyotosheleza ya mikopo na ugavi | Kahawa inauzwa kwa Dola za Marekani | Kuzuka kwa wadudu wapya na magonjwa |
| Upatikanaji wa aina bora za kahawa zinazohimili CBD, CLR na CWD | Fedha ya Tanzania inayoyumba | Ongeza ufadhili wa wadau katika majukumu shirikishi ya tasnia | Kubadilika badilka kwa bei za kahawa katika soko la dunia |
| Soko huria la kahawa | Miundombinu mibovu | Uwezekano wa kuendeleza Robusta zilizooshwa | Kuibuka kwa viwango vya ziada vya uthibitishaji |
| Utayari wa wadau kusaidia na kufadhili utafiti wa kahawa | Usambazaji wa taarifa za soko usiotosheleza | Uwezekano wa kuongeza unywaji wa ndani | Ushindani na mazao mengine |
| Mazingira mazuri ya kisiasa | Mazingira ya biashara yanaweza kuboreshwa | Taasisi za mafunzo kuhusu kilimo cha mazao | Viwango vya juu vya riba |

Chanzo: Uchanganuzi wa Bodi ya Kahawa, Mikutano ya Wadau, 2010

## Kiambatanisho cha 2: Maazimio ya Mkutano wa Kitaifa wa Kahawa (2011)

Maazimio ya Mkutano wa Kitaifa wa Kahawa uliofanyika katika Hoteli ya Oasisi, Morogoro tarehe 26-27 Mei, 2011

1. Wadau wameishukuru serikali kwa kutoa ruzuku ya pembejeo za kahawa.Wameahidi kutumia fursa hiyo katika kuongeza uzalishaji na ubora wa zao la kahawa nchini

2. Wadau wamepongeza na kuwashukuru wote walioratibu na kuandika mkakati wa kuendeleza zao la kahawa na umepokelewa kwa sauti moja(wajumbe 121 wamekubali na 3 wameukataa-demokrasia imezingatiwa)

3. Wadau wameshauri kwamba ili mkakati uweze kutekelezwa vyema,itengenezwe programu kabambe itakayoainisha ushiriki wa wadau wote na namna ya kuugharamia na hususani majukumu yetu ya pamoja

4. Wadau wameazimia kwamba halmashauri za wilaya ziangalie zitakavyoweza kuchangia angalau asilimia 20 ya mapato yanayotokana na kahawa katika kuendeleza tasnia ya kahawa

5.TaCRI waanze kufanya utafiti utakao jibu changamoto zinazoikabili tasnia ya kahawa nchini kama vile ukame kwa kutafiti aina mpya za kahawa zitakazohimili mabadiliko ya tabia nchi.

6. Mkutano huu pia umepokea kwa moyo wa shukrani uamuzi wa serikali wa kuendelea kuwekeza katika utafiti wa zao la kahawa

7. Bodi ya Kahawa iratibu kufanyika kwa tathimini itakayoangalia kwa undani namna nzuri ya kufanya biashara ya zao la kahawa ili iwe ya haki na ushindani wenye tija kuanzia uzalishaji shambani hadi hatua ya kuuza katika minada (value chain analysis)

8. Wajumbe walikubaliana kuwa uchangiaji wa mfuko wa kahawa uwe kwa kilo inayouzwa badala ya asilimia ya bei

9.Wakulima bora wa kahawa watambuliwe na wazawadiwe katika mkutano wa wadau na katika sherehe za kitaifa hususani sherehe za NaneNane

10. Mkutano umekubaliana kwa pamoja kuanzisha mfuko wa kuendeleza zao la kahawa na kuunda kamati ya wadhamini (Board of Trustees) itakayoshughulikia uanzishwaji wa mfuko huo. Wajumbe hao wamepewa mamlaka ya kukamilisha uandaaji wa nyaraka zinazohusiana na usajili wa mfuko.Aidha uchangiaji wa viwango vipya utaanza msimu wa 2011/2012. Kabla ya hapo uchangiaji kwa viwango vya zamani utaendelea. Wajumbe wake ni kama ifuatavyo:

Wajumbe wawakilishi wa wakulima: Gabriel Ulomi, Andrew Kakama, Hyasinth Ndunguru
Mwakilishi wa Halmashauri: Hilda Lauo
Mwakilishi wa Wizara ya Kilimo: Geoffrey Kirenga
Mwakilishi wa wafanyabiashara (TCA): Amir Hamza na Yoel Yatera
**Settlers**: Wizara ya Kilimo (KM) na TCB

- Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika na Bodi ya Kahawa Tanzania

## Kiambatanisho cha 3: Muhtasari wa Michango ya Kamati za Kanda za Wadau

**Kampeni kwa ajili ya Kuongeza Uzalishaji wa Kahawa**

**Mkutano wa Kwanza wa Wadau wa Kanda**

**Aprili hadi Juni, 2009**

**Taarifa ya Mwisho**

**Usuli**

Mojawapo ya majukumu ya TCB ni kuwezesha mipango mkakati ambayo itaongeza tija. Katika mwaka 2006, kulikuwa na uzinduzi wa kampeni ya kitaifa ya kuongeza uzalishaji wa kahawa, kwa agizo kutoka kwa Waziri Mkuu wa wakati huo, kwamba uzalishaji unapaswa kufikia tani 120,000 kabla ya 2010. TCB wameitikia changamoto hii kwa kutafuta kuwahusisha wadau wa kila mojawapo ya kanda za kahawa katika mchakato shirikishi ambao utahitimishwa kwenye kutengeneza mpango mkakati wa kuongeza tija katika eneo lao.

Uhamasishaji wa awali uliendeshwa na Mkurugenzi Mkuu wa TCB katika kanda zote, na wadau wakuu walibainishwa kushiriki katika michakato hii ya upangaji. Matokeo ya pamoja yatautaarifu mkutano wa Kitaifa wa Wadau wa Kahawa utakaoendeshwa baadaye mwaka huu

Kwa mzunguko wa awali wa mikutano ya wadau, TCB iliungana na Mtandao wa Kusaidia Bidhaa Endelevu “Sustaniable Commodities Assistance Network (SCAN) na “Cafe Africa.” Wafanyakazi watatu wa TCB kutoka idara ya uendelezaji wa zao la Kahawa walichukua jukumu la jumla la kupanga, usafirishaji, utekelzaji na utoaji wa taarifa.

Mikutano saba ilifanyika ikihusisha mikoa minane: Arusha, Manyara, Kilimanjaro, Iringa, Mbeya, Kagera,Kigoma na Ruvuma. Mikutano hii ilihudhuriwa na wadau 600, kutoka wilaya 28 wakiwakilisha sehemu zote za mnyororo wa thamani. Mikutano hiyo iliwezeshwa kwa njia shirikishi na kuwapatia wadau nafasi ya kubainisha fursa na changamoto kwenye kuongeza tija katika maeneo makuu manne: uzalishaji, usindikaji, masoko na masuala ya kimuundo.

**Malengo ya Mkutano wa Wadau**

- Ubainishaji wa wadau juu ya fursa na changamoto katika kuongeza uzalishaji katika mkoa wao
- Kuwasaidia wadau katika maendeleo ya mipango mkakati ya kimkoa yenye uhalisia na inayowezekana
- Kuwapatia wadau taarifa za msingi, kuhusu sekta ya kahawa kiulimwengu na kitaifa
- Kuboresha upatikanaji wa takwimu zinazoaminika ambazo zitaarifu majukwaa ya kimikoa na kitaifa na kusaidia kufanya uamuzi na upangaji wa rasilimali.

**Matokeo Yaliyotarajiwa kwa Mkutano wa Kwanza:**

- Makubaliano kuhusu wadau wakuu ni nani na kuhakikisha sehemu zote za mnyororo wa thamani zinawakilishwa
- Mwafaka kuhusu zipi ni fursa muhimu na changamoto za mkoa
- Kukubaliana hatua zinazofuata katika kuanzisha mpango mkakati kwa mkoa
- Kamati ya mkoa ya wadau ichaguliwe kutekeleza hayo hapo juu, kwa kuwezeshwa na TCB.

**Changamoto kuu katika kuleta tija:**

Kulikuwa na masuala mbalimbali ambayo yalikuwapo katika mikutano yote ya wadau, baadhi yake yalikuwa mahususi kwa kanda mojamoja. Masuala hayo yanaakisiwa katika taarifa mojamoja na yatashughulikiwa kupitia mipango mkakati ya kikanda. Hata hivyo, kulikuwa na masuala kadhaa ambayo yalikuwa ya kawaida kwa mikutano ya wadau, na hivyo yanahitaji uchanganuzi na mafikirio zaidi kuhusu jinsi ambavyo kanda hizo zinaweza kusaidiwa kupitia jitihada za sera ya taifa. Changamoto hizi zilikuwa ni:

- Huduma dhaifu za ugani: ukosefu wa maofisa, ukosefu wa wataalamu wa kahawa, kutokuwezeshwa
- Kutokupata pembejeo wanazozimudu: gharama za juu za mbolea, uhalisia, upatikanaji wa mikopo kwa wakati.
- Upatikanaji mdogo wa miche bora ya kahawa
- Ukosefu wa taarifa za soko kwa wakulima wadogowadogo
- Ushuru wa Wilaya: NI mkubwa mno na kukosekana kwa mashauriano na wadau
- Miundombinu mibovu: Barabara (barabara, reli, bandari, mawasiliano, intanet)

**Masuala ya Kitaasisi kwa TCB:**

Karibu katika kila mkutano, jukumu na wajibu wa TCB vilizungumziwa, hususan kuhusu majadiliano juu ya changamoto za kitaasisi na kimpangilio ili kuleta tija. Hizi ni pamoja na:

- Ucheleweshaji katika malipo
- Ucheleweshaji katika mchakato wa maombi ya leseni
- Ucheleweshaji wa muda mrefu katika uchanganuzi wa sampuli
- Leseni nyingi
- Kanuni ya utoaji wa leseni ya kazi inayotumika sasa bila ya muda wa nyongeza
- Uwezekano wa mgongano wa majukumu, k.m TCB ni chombo cha udhibiti lakini kinakusanya mapato kwa niaba ya LGAs
- Ukosefu wa taarifa kuhusu bei
- TCB iko mbali mno na wadau wake; ni vizuri kungekuwa na Mratibu wa Kahawa katika kila wilaya.

Mrejesho huu unapaswa kuangaliwa katika mtazamo chanya, kwa vile tayari Bodi inafanyia kazi masuala kadhaa ya hapo juu. Mkutano wa wadau huipa Bodi fursa ya kuwasikiliza wateja wake moja kwa moja na kuingiza katika mkondo na kurekebisha huduma kuzifanya zitoe mwitikio zaidi kwa wadau na kuhakikisha mazingira yanayowezesha yanajengwa kwa ajili ya tasnia ya kahawa. Mikutano yote ya kanda ilifurahishwa na mikutano ya wadau, na kuomba ifanyike mara kwa mara.

**Masuala yaliyogundulika na wawezeshaji:**

1. Kuna maeneo ya msingi ambayo hayakujumuishwa na mikutano ya wadau, lakini yanahitaji kazi ya maandalizi ya kuyatathmini na kuwabainisha wadau. Maeneo hayo ni pamoja na Rukwa, Tanga, Morogoro na Mwanza.
2. Posho na malipo ya safari vilileta ubishi katika kanda kadhaa. Ili kuhakikisha umiliki na uendelevu, ni muhimu kufikia makubaliano na LGA ya jinsi ambavyo wakulima wao watawezeshwa kushiriki.
3. Uchanganuzi wa hali kwa Kilimanjaro haukukamilishwa kwa kina kama katika Kanda nyingine, kutokana na kutokuwepo kwa uwakilishi wa sehemu zote za mnyororo wa thamani. Kutokana na umuhimu wa Kilimajaro kama habu ya tasnia hii, TCB inapaswa kuchukua mtazamo tofauti kwa kanda nyingine na kuishughulisha sekta binafsi katika ushiriki. Uchanganuzi wa hali unapaswa kupitiwa na kuimarishwa katika mikutano ya wadau itakayofuata.
4. Msukumo ulioanzishwa kupitia mikutano ya wadau unapaswa utumiwe kama msingi na ufuatiliaji kusaidia kamati katika kupanga ufanyike haraka kadiri inavyowezekana.

**Hatua Zinazofuatia:**

- TCB isaidie kamati kuandaa rasimu ya mipango (tazama pendekezo la mpango kazi Kiambatisho cha 1)

- Uchanganuzi na ujumuishaji wa mipango ya kanda katika mpango wa kitaifa

- Maandalizi ya Mkutano wa Kitaifa wa Wadau

**UCHUNGUZI NA MAONI KWA AJILI YA KUJUMUISHWA KATIKA MKAKATI**

| KANDA | UCHUNGUZI | MAONI/MAPENDEKEZO |
|---|---|---|
| **KAGERA** | Mkakati uweke wazi lengo la kila wilaya ili mipango ya utekelezaji ipangwe kufikia lengo | Itatekelezwa chini ya programu |
| | Mkakati uweke lengo la kubadilisha mfumo wa kuuza kahawa ya maganda na kuuza kahawa iliyokobolewa tu | Tumejumuisha katika mkakati huu kama kipengele kipya chini ya **5.2.1**<br><br>Kusambaza taarifa kwa wazalishaji kuhusu manufaa ya kahawa iliyokobolewa nyumbani<br>Kuanzisha sera inayotawala ukoboaji wa nyumbani<br>Kuwapatia wamiliki wadogowadogo mafunzo ya kuanzisha na kuendesha inayofaa ukoboaji wa nyumbani<br>Kushawishi kwa ajili ya msaada wa dhamana ya uwekezaji wa matumizi ya mtaji katika ukoboaji wa nyumbani |
| | Kuanzisha mfumo wa kahawa za kuosha za Robusta na Arabika mkoani Kagera | Kahawa ya Robusta iliyooshwa bado iko katika majaribio, hivyo haikujumuishwa katika mkakati huu<br>Tayari Arabika imejumuishwa katika mkakati huu |
| | Mkakati uwe na lengo la makusudi kuwaelimisha wakulima wa Kagera waanze kutumia mbolea | Imekwishajumuishwa katika mkakati, hivyo haikufikiriwa |
| | Mkakati uweke lengo la kuongeza ubora wa kahawa ya Robusta kwa kuongeza jitihada za kukoboa kahawa ngazi ya kaya | Tayari imekwishajumuishwa katika mkakati kama **5.2.1** hapo juu |
| | Mkakati uweke mazingira yatakayowezesha mfumo wa biashara wa kahawa wa Tanzania kushindana na wa nchi jirani | Imefikiriwa chini ya **5.3.1**<br><br>(e) Kuchunguza fursa za kupunguza bei za usafiri , ufungashaji wa vifaa na ushuru wa nishati<br><br>(g) Kuboresha ushindani wa shambani |

| | | |
|---|---|---|
| | | |
| | Mkakati uwe na lengo la makusudi kuwaelimisha wakulima wa Kagera waanze kutumia mbolea | Tayari iko katika mkakati |
| | Mkakati uweke lengo la kuongeza ubora wa kahawa ya Robusta kwa kuongeza jitihada za kukoboa kahawa ngazi ya kaya | Tayari imekwishajumuishwa hapo juu |
| | Mkakati uweke mazingira yatakayowezesha mfumo wa biashara ya kahawa wa Tanzania kushindana na nchi jirani | Tumejumuisha chini ya **5.3.1**<br><br>1(e) Kuchunguza fursa za kupunguza gharama za usafiri, ufungashaji wa vifaa na ushuru wa nishati<br><br>1 (g) Kuboresha ushindani wa bei shambani |
| | Ni vyema mkakati ukasema chanzo cha fedha kuutekeleza | Hili litajumuishwa wakati wa utekelezaji baada ya kubainisha chanzo cha fedha/wafadhili |
| | Mkakati huu ni mzuri na umezingatia karibia changamoto zote zinazoikabili sekta ya kahawa | |
| **KIGOMA** | Kamati inapendekeza upitishwe kwa ajili ya maendeleo endelevu ya Sekta ya Kahawa | |
| | Upanuzi wa maeneo ya uzalishaji kilimo cha kahawa | Tayari imekwishajumuishwa katika mkakati huu |
| **RUKWA na** | Uzalishaji wa miche bora ya kahawa | Tayari umekwishajumuishwa katika mkakati huu |
| | Utafiti wa maeneo yanayofaa kwa kilimo cha kahawa na soko | Tayari imejumuishwa katika mkakati huu |

| | | |
|---|---|---|
| **MBEYA** | Miongozo itolewe ya kurudisha asilimia ya fedha iliyokusanywa kwenye ushuru wa kahawa kuendeleza zao. | Ilikubaliwa kwamba kila halmashauri ya wilaya ichangie walau 20% ya ushuru wa kahawa kusaidia shughuli za kahawa katika wilaya hiyo. Hivyo**, 6 1e** chini ya serikali za mitaa inapaswa isomeke: Serikali za Mitaa katika kila mkoa unaozalisha kahawa zina majukumu ya kutumia rasilimali na fedha kwa ajili ya kahawa kupitia mipango yao ya maendeleo ya kilimo na bajeti angalau 20% ya ushuru wa kahawa. |
| | Kufikia mwaka 2020 kahawa zote zikobolewe kupitia viwanda vya kati (CPU) | Tayari katika Mkakati |
| | Wizara ya Kilimo kwa kushirikiana na Bodi ya Kahawa isimamie kutatua mgongano wa maamuzi uliopo kuhusu ununuzi wa kahawa mbichi unaofanywa na Makampuni binafsi | Iko chini ya kanuni za kahawa |
| | Kuwe na ruzuku ya pembejeo na dawa kwa zao la kahawa | **Chini ya 5.1.1 kati ya a na c**<br><br>**b) Anzisha ruzuku kwa pembejeo za kahawa** |
| **RUVUMA** | Kuwepo na Ruzuku kwenye dawa na mbolea za kahawa | Tayari imejumuishwa chini ya Rukwa na Mbeya chini ya **5.1.1.** |
| | Kuanzisha siku ya kahawa kitaifa | **1e) Anzisha siku ya Kitaifa ya kahawa chini ya 5.5.1** |
| | Serikali irudishe mafungu ya uwezeshaji (A-CBG) na ugani (A-EBG) kwenye mfuko wa DADPS | Imekwishajumuishwa katika mkakati huu na itafikiriwa katika programu |
| | Kahawa ya Mbinga iuzwe kama ya Mbinga ya zamani badala ya Makambako ya zamani ili kupunguza gharama za usafirishaji wa kahawa kwa mkulima. | Iko chini ya mamlaka ya TCB **(Kazi za udhibiti)** |

| | | |
|---|---|---|
| | Halmashauri za wilaya zirudishe kiasi cha fedha za ushuru wa kahawa kwenye shughuli za kuendeleza uzalishaji wa kahawa kwa mfano wa Mbinga | Tayari imejumuishwa |
| | Serikali irejeshe vifungu vya ugani na uwezeshaji kwemye mfumo wa DADP | Tayari imejumuishwa |
| **IRINGA** | TaCRI itoe mgawanyo sawa wa miche ya vikonyo na msisitizo uwekwe kwenye maeneo mapya ya uzalishaji kama Mkoa wa Iringa na Njombe | Kufikiriwa chini ya programu |
| | TaCRI ianzishe kituo kidogo kwa huduma za Mkoa wa Iringa | Kufikiriwa chini ya programu |
| **MARA** | Rasimu imeandaliwa kwa kiingereza, ni vema itafsiriwe kwa Kiswahili | Tayari imekwishatekelezwa |
| | Ni vyema kuwepo na ruzuku ya pembejeo za kahawa kama inavyotolewa kwenye mazao ya chakula | Imekwishajumuishwa |
| | Bodi ya kahawa isimamie masoko katika maeneo mapya ya uzalishaji ili kuvutia wanunuzi, mfano. Ukerewe, Musoma | Iko chini ya kanuni za kahawa |
| | Bodi ya kahawa/Serikali itoe mwongozo juu ya kurudisha sehemu ya mapato yanayotokana na ushuru kwa wakulima; mfano 20% | Tayari imekwishazingatiwa |
| | Kuwepo na wazalishaji miche kibiashara | Kuzingatiwa chini ya programu |
| **ARUSHA na MANYARA** | Wizara itoe mwongozo unaoziagiza halmashauri za wilaya kutoa kipaumbele kwa kahawa katika DADP | Imekwishaingizwa katika mkakati huu |
| | Utaratibu wa elimu kwa mkulima mmoja mmoja urudiwe na kuzingatiwa | Kuzingatiwa chini ya programu |
| | Kuwepo na Ruzuku ya | Tayari imezingatiwa katika mkakati |

| | | |
|---|---|---|
| | pembejeo za kahawa | huu |
| | Mawakala na wasambazaji wa pembejeo za kahawa wasajiliwe na kuratibiwa | Tayari iko katika makakti huu chini **ya 5.1.1 2b** |
| | Halmashauri za wilaya zitenge asilimia moja ya fedha zitokanazo na ushuru wa kahawa ili zitumike kuendeleza shughuli za ugani | Tayari imejumuishwa chini ya mamlaka ya serikali za mitaa **6. 1e** ingawa asilimia iko juu zaidi kuliko asilimiai iliyopendekezwa na kanda za Manyara na Arusha |
| | Kila mkulima wa kahawa asajiliwe/atambulike | Iko chini ya kanuni za kahawa |
| | Wakaguzi wa kahawa wawezeshwe na kufuatiliwa na Bodi ya kahawa | Kufikiriwa chini ya programu |
| | Wakulima wapya wa kahawa wapewe ushirikiano | Tayari imejumuishwa chini ya sera ya mazingira |
| | Uwezeshaji wa kilimo cha umwagiliaji na uvunaji wa maji ya mvua uonekane katika mkakati | Tayari imezingatiwa chini ya **5.1.1**<br><br>Kuanzisha na kusaidia mifumo ya kilimo cha umwagiliaji kati ya **c na d** |
| | Kuwepo na | |
| | Kamati ya Kitengo ya Uendeshaji | Wawakilishi wawili (Mwenyekiti na Katibu) kutoka NSC |
| | Kamati ya Taifa ya Wadau | Wawakilishi wawili (Mwenyekiti na katibu) kutoka ZSC |
| | Mkutano wa wadau wa kanda | Mwenyekiti na katibu watachaguliwa na wanachama katika kila kanda |
| | Mkulima wa kahawa hapati elimu ya kutosha, utaraitibu wa huduma ya ‘mkulima hadi mkulima’ ujaribiwe | Kuzingatiwa chini ya programu |
| **KILIMANJARO** | Wakulima wapewe ruzuku za pembejeo moja kwa moja kama ilivyo kwa pamba na korosho | Tayari imejumuishwa |
| | Uwezeshaji kilimo cha umwagiliaji na uvunaji wa maji ya mvua utajwe katika mkakati | Tayari imejumuishwa |
| | Kufanyike mikataba ya watu binafsi au taasisi kuzalisha miche | Tayari imejumuishwa |
| | Njia ya uzalishaji kwa chupa | Kuizingatia hii chini ya programu |

| | | |
|---|---|---|
| | ifanyike hapa nchini kwa mfano maabara za Mikocheni, SUA, Tengeru ambazo zinaweza kuzalisha miche milioni 20 au zaidi kwa mwaka | lakini inahitaji uchanganuzi wa kina |
| | Usindikaji wa kahawa nyumbani uwe 'uondoshwe.'<br><br>Katika mwaka wa kwanza wa utekelezaji wa mkakati kila mkulima aandikishwe | Tayari imezingatiwa chini ya zilizooshwa kikamilifu<br><br>Kuzingatiwa chini ya kanuni za kahawa |
| | Wakaguzi wa kahawa wawezeshwe na kufuatiliwa na Bodi ya kahawa | Tayari imezingatiwa |
| | Kuwepo na mkutano wa wadau wa kahawa ngazi ya mkoa badala ya kanda na taifa tu. | Kuzingatia chini ya muundo wa utekelezaji |
| | Kutafutwe chanzo kingine cha fedha za kutekeleza mkakati huu. Isitegemewe ASDP tu. | Chanzo cha fedha kuamuliwa katika pro1gramu hii |
| `` | Ofisa Ugani atakayetoa mkulima bora katika mashindano ya kahawa naye azawadiwe | Kufikiriwa na TCB |
| | SACCOs na AMCOs ziimarishwe ziweze kuwakopesha wakulima wa kahawa pembejeo za kilimo. | Tayari umejumuishwa katika mkakati huu |

## Kiambatanisho 4

**Viambatanisho (Vinapatikana kwa maombi, kama waraka tofauti)**

| | |
|---|---|
| Kielelezo cha 1 | Nusu ya kahawa ya dunia huzalishwa na Brazil na Vietnam |
| Kielelezo cha 2 | Mahitaji ya Robusta yanakua kwa haraka zaidi kuliko mahitaji ya Arabika |
| Kielelezo cha 3 | Kahawa za Arabika laini zinaongezeka zaidi ya bei za Asilia na Robusta |
| Kielelezo cha 4 | Magunia milioni ishirini na tano ya Arabika yameuzwa kwa bei ya juu Ikilinganishwa na New York C |
| Kielelezo cha 5 | Soko mahususi laweza kufikia magunia milioni 19 ifikapo mwaka 2020 |
| Kielelezo cha 6 | Tasnia ya kahawa inaelekea haraka kwenye viwango endelevu |
| Kielelezo cha 7 | Uzalishaji wa kahawa ya Tanzania umedumaa |
| Kielelezo cha 8 | Uzalishaji wa Arabika unapungua wakati uzalishaji wa Robusta unaongezeka |
| Kielelezo cha 9 | Ushukaji wa jumla katika usafirishaji nje wa Arabika unatokana na anguko kali huko Kaskazini |
| Kielelezo cha 10 | Ingawa bei ni za chini, lakini usafirishaji nje wa Robusta umeongezeka |
| Kielelezo cha 11 | Wanunuzi watano wanawakilisha 70% ya usafirishaji nje wa kahawa , ambazo hasa zinakwenda Japan |
| Kielelezo cha 12 | Tanzania ina fursa ya kuongeza uzalishaji mara mbili zaidi |
| Kielelezo cha 13 | Asilimia arobaini na tano ya Arabika ya Tanzania hupata thamani ya juu kulinganisha na New York |
| Kielelezo cha 14 | Matumizi mazuri ya viwanda vya kati (CPUs) yanaweza kupunguza gharama na kuongeza pato la mkulima |
| Kielelezo cha 15 | Vikundi vya wakulima vinaelekea kujihakikishia mapato bora zaidi kwa wakulima wao |
| Kielelezo cha 16 | Mazingira ya biashara ya Tanzania si mazuri kulinganisha na wazalishaji wakubwa wa kahawa duniani |
| Kielelezo cha 17 | Kukosekana kwa ufanisi katika muda wa usafirishaji husababisha kuporomoka kwa bei, hususan kwa kahawa yenye ubora wa hali ya juu |
| Kielelezo cha 18 | Uzalishaji wa Kahawa ya Tanzania ungeweza kuwa mara mbili zaidi ifikapo 2020 |
| Kielelezo cha 19 | Uzalishaji wa Kahawa Tanzania unaweza kufikia kg 600 kwa hekta |
| Kielelezo cha 20 | Makadirio ya uzalishaji wa miche ni miche milioni 75 ifikapo 2012 |
| Kielelezo cha 21 | Kahawa iliyotayarishwa kupitia viwanda vya kati (CPU) inaweza kuzidi viwango vya sasa vya uzalishaji ifikapo 2020 |
| Kielelezo cha 22 | Kahawa iliyotayarishwa kupitia viwanda vya kati (CPU) |